BURIANI MASHUJAA WETU



YANA MWISHO HAYA

TAARIFA KWA UMMA YA NDG. LUHAGA JOELSON MPINA, KUHUSU UCHAMBUZI WA MUHTASARI WA RIPOTI YA TUME YA RAIS YA KUCHUNGUZA MATUKIO YA GHASIA NA UVUNJIFU WA AMANI YALIYOTOKEA WAKATI NA BAADA YA UCHAGUZI MKUU OKTOBA 2025, LEO TAREHE 1 JUNI 2026, DAR ES SALAAM.

JUNI, 2026

YALIYOMO

1. UTANGULIZI....1
2. CHANZO NA VICHOCHEO VYA MAANDAMANO....3
3. UHALALI WA VITENDO VYA SERIKALI WAKATI WA KUTULIZA GHASIA....19
4. VITENDO VYA SERIKALI BAADA YA MATUKIO YA MAUAJI YA OKTOBA 2025....24
5. UHALALI WA MAANDAMANO YA OKTOBA 2025....31
   (I) Madai ya kuwa Waandamanaji hawakutoa taarifa polisi....32
   (II) Madai ya kwamba eti Waandamanaji walizuia haki ya mpiga kura....32
   Upande wa CCM. 33
   Upande wa ACT Wazalendo....34
   Upande wa CHADEMA....37
   Mazingira ya Uchaguzi....38
   (III) Madai ya kwamba Waandamanaji walikuwa na silaha (Bunduki)....41
   (IV) Madai ya kwamba Maandamano yalihatarisha usalama wa Taifa....42
   (V) Madai ya Waandamanaji walikuwa wafuata mkumbo....43
5. MASUALA YA KIUCHUMI....44
6. JUMUIYA ZA KIMATAIFA....48
7. UWAZI NA UWAJIBIKAJI KUHUSIANA NA MAUAJI YA OKTOBA 2025....49
8. HITIMISHO....53
9. MAONI NA MAPENDEKEZO....65

TAARIFA KWA UMMA YA NDG. LUHAGA JOELSON MPINA, KUHUSU UCHAMBUZI WA MUHTASARI WA RIPOTI YA TUME YA RAIS YA KUCHUNGUZA MATUKIO YA GHASIA NA UVUNJIFU WA AMANI YALIYOTOKEA WAKATI NA BAADA YA UCHAGUZI MKUU OKTOBA 2025, LEO TAREHE 1 JUNI 2026, DAR ES SALAAM.

1. UTANGULIZI

Ndugu Waandishi wa Habari, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu mwingi wa Rehema muumba mbingu na nchi kwa kutujalia uhai na afya njema kuweza kukutana siku ya leo tarehe 1 Juni 2026 hapa jijini Dar es Salaam.

Pili nichukue nafasi hii kutoa pole nyingi kwa Familia ya **Mzee Joseph Magufuli Marco Nyahinga** na watanzania kwa ujumla kufuatia kifo cha **Mama Suzana Ngolo Mussa Magufuli** mama yake mzazi na aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, **Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** kilichotokea tarehe 25 Mei 2026 na kupumzishwa kwenye nyumba yake ya milele Tarehe 29 Mei 2026 huko Chato, Geita. Heri tumbo lililokuzaa na matiti uliyonyonya Dk. Magufuli pumzika kwa amani Mama yetu kipenzi umetoa mchango mkubwa kwenye Taifa.

Aidha niwashukuru ninyi Ndugu Waandishi wa Habari kwa nafasi hii mliyonipa ili niweze kutoa maoni na mapendekezo yangu baada ya kufanyia uchambuzi muhtasari wa Ripoti Tume ya Rais ya kuchunguza matukio ya ghasia na uvunjifu wa amani yaliyotokea wakati na baada ya uchaguzi mkuu Oktoba 2025 iliyoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, **Mheshimiwa Mohamed Chande Othman** iliyowasilishwa kwa Rais tarehe 23 Aprili 2026.

Mtakumbuka kuwa mnamo tarehe 21 Januari 2026 nilipokea barua rasmi ya mwaliko wa kuhudhuria mbele ya Tume ya Jaji Chande kwa ajili ya majadiliano tarehe 31 Januari 2026, Niliwajibu Tume kwa barua ya tarehe 30 Januari 2026 kuwa sitaweza kuhudhuria kikao hicho kwa kuwa tume hiyo sio huru na ripoti yake haitaaminika kitaifa na kimataifa. Msimamo huu pia ndiyo ulikuwa msimamo wa Chama changu cha ACT Wazalendo na hata Vyama vingine kama CUF na CHADEMA. Muhtasari wa ripoti ya Tume ya Jaji Chande umedhihirisha ukweli wa kile tulichokiamini awali.

Tangu kuwasilishwa kwa ripoti ya Jaji Chande, nimekuwa nikipokea simu nyingi za wananchi na Waandishi wa Habari kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi wakitaka kujua maoni na mapendekezo yangu kuhusu ripoti ya Tume ya Jaji Chande ambapo pamoja na ukweli kwamba chama changu cha ACT Wazalendo kimeshatoa matamko ya chama ya **Tarehe 9 Novemba 2025, Tarehe 19 Januari 2026 na Tarehe 4 Mei 2026** ambapo matamko yote nayaunga mkono.

Lakini na mimi kama mwanachama niliyepewa dhamana ya kupeperusha bendera ya Chama cha ACT Wazalendo kuwania nafasi ya juu kabisa ya uongozi wa nchi yetu kuwa mgombea Urais nikaona leo ni siku muafaka ya mimi kutoa Maoni yangu kuhusiana na Ripoti ya Jaji Chande.

Pia natambua juhudi za wananchi na Taasisi mbalimbali waliojitokeza hadharani kutoa Maoni yao kuhusu ripoti ya Jaji Chande akiwemo Jaji Joseph Sinde Warioba, Prof. Anna Tibaijuka,

Mzee Samweli Kassori, Wakili Peter Madeleka, TLS, LHRC, Asasi za Kiraia 14, UDASA na Chama cha CHADEMA.

Kabla sijaanza kuchambua kipengele kwa kipengele yako mambo ya kiujumla kama ifuatavyo:-

(i) Muhtasari wa Ripoti ya Tume ya Jaji Chande kwa sehemu kubwa umejaa simulizi badala ya ushahidi wa vielelezo na uthibitisho wa kisayansi, una takwimu na taarifa zinazokinzana na umeacha kuchambua na kufanya utafiti wa masuala muhimu ambayo jamii ilikuwa na shauku kubwa kuyafahamu.

(ii) Tume kwa kiasi kidogo imezingatia maoni ya wananchi na imeyakubali maudhui ya tathmini ya uchaguzi niliyoitoa mnamo tarehe 6 Disemba 2025 yenye kichwa cha habari "Taarifa kwa Umma ya Ndugu Luhaga Joelson Mpina kuhusu Shauri la kesi ya Rufaa, Uchaguzi Mkuu na Maandamano ya tarehe 29 Oktoba 2025"

2. CHANZO NA VICHOCHEO VYA MAANDAMANO

Muhtasari wa Ripoti ya Jaji Chande umebainisha mambo 5 yenye vipengele 20 kuwa ndiyo chanzo kikuu cha ghasia na machafuko ya tarehe 29 Oktoba 2025, katika hili nawapongeza Tume kubaini kuwa utendaji dhaifu wa Serikali ya awamu ya 6 ndiyo chanzo kikuu cha machafuko na vifo Oktoba 2025, asante sana Tume kwa kuona na kuweka wazi ukweli huo ambao umefichwa kwa gharama kubwa kwa kipindi miaka 5 kwa kampeni za utapeli za **4Rs, *"Mama Hana Deni, Mama hatukudai".*** Hakika ***mwisho wa ubaya ni aibu*** na ***lakuvunda halina ubani.*** Wakati naipinga kampeni hii haramu hadharani ndani na nje ya Bunge

nilipigwa vita na kutengenezewa chuki kubwa na baadhi ya Viongozi waandamizi wa Chama cha Mapinduzi na Serikali. Leo Tume ya Jaji Chande imethibitisha na mmewasikia wabunge huko Dodoma nao wanalia hawajui fedha za ujenzi wa barabara na miradi mingine zimekwenda wapi.

Hivyo nami nakubaliana na Tume ya Jaji Chande kama ifuatavyo:-

2.1 Yapo masuala ya kisiasa yanayohusishwa na madai ya Katiba Mpya, Demokrasia katika mfumo wa Vyama vingi vya Siasa, malalamiko ya kuingiliwa ndani ya Vyama vya Siasa, madai ya maboresho ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na mfumo mzima wa uchaguzi. Kwa mfano:-

(i) Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Msajili wa Vyama vya Siasa (RPP), Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) na Mahakama zinatumika na Chama cha Mapinduzi na mtawala kuwaengua wagombea wa upinzani wa nafasi za Rais, Wabunge na Madiwani kwa mabavu na kinyume cha Sheria.

(ii) Katiba na Sheria za uchaguzi zinakandamiza Vyama vya upinzani ikiwemo kuweka masharti ya kutopingwa matokeo ya uchaguzi wa Rais mahakamani na kuipa nguvu Tume kuwa rufaa ya mwisho katika mapingamizi ya nafasi ya Rais ili kufanikisha kuwaengua wapinzani. Kifungu cha 37 (6) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024. Kuandaa kanuni za maadili zinazokinzana hadi na Katiba ya nchi.

2.2 Masuala ya Kiuchumi yanayojumuisha ugumu wa maisha, ukosefu wa ajira na kukosekana kwa usawa katika fursa za ajira

na za Kiuchumi, mazingira ya biashara na uwekezaji yasiyo rafiki, utitiri wa kodi na tozo na mfumo usio rafiki wa utozaji na ukusanyaji wa mapato.

Ni kweli kabisa wananchi wana hasira kubwa na Serikali ya awamu ya 6 kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kuhusu kupanda kiholela kwa bei za bidhaa na huduma muhimu za wananchi kama nishati ya mafuta, umeme, maji, gesi, mbolea, sukari, gharama za matibabu, bidhaa za afya, vifaa vya ujenzi, pembejeo, mbegu, Nauli nk. Kwa mfano hivi sasa licha ya kuwepo akiba ya mafuta yanayotosheleza miezi 3 ijayo lakini Serikali imeruhusu Dizeli na Petroli kupanda kiholela kwa zaidi ya Tsh. 1,200 kwa lita kwa kisingizio cha kupanda bei katika soko la dunia.

Kipindi bei ya mafuta ilipopanda kwenye soko la dunia Serikali ilitoka hadharani kutangaza kupanda kwa bei za bidhaa lakini leo bei ya mafuta imeshuka katika soko la dunia kutoka Dola 112.9 hadi kufikia Dola 87.3 kwa pipa takriban bei imeshuka kwa 22% leo ni siku ya 5 hakuna tamko kutoka serikalini kuhusu bei mpya ya mafuta na bidhaa.

(ii) Ukosefu wa ajira, Vijana zaidi ya 800,000 sawa na 80% ya vijana wanaoingia katika soko la ajira hukosa ajira kila mwaka na kwamba ajira zao zimekuwa zikihujumiwa kuhamishwa na kupewa raia wa kigeni. Mifumo ya ajira haiko wazi na imejaa upendeleo wa kila aina kwa misingi ya Ndugu, jamaa na marafiki.

Changamoto nyingine ni pamoja na kukosa mitaji, mikopo yenye masharti nafuu, mikataba ya ajira, huduma ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Bima, mipango bora ya wastaafu na kukosekana kwa taasisi ya ajira kwa vijana.

Viongozi wanapatikana kwa misingi ya upendeleo uliopitiliza na unaweza kukuta mkoa mmoja una Makatibu Wakuu zaidi ya 10, Mawaziri zaidi ya 5, Mabalozi wengi huku mikoa mingine ikiwa haina hata Katibu Mkuu wala Waziri mmoja. Mara nyingi kupata ajira mpaka uwe na **Godfather** serikalini, kwa Serikali ya aina hii **Gen-Z** hawawezi kuacha kuandamana kudai haki.

(iii) Kiuchumi, wakulima kupunjwa bei ya mazao yao kwa maslahi binafsi ya baadhi ya Viongozi waandamizi serikalini ikiwemo kusingizia anguko la soko la dunia, ushuru na makato makubwa, stakabadhi ghalani, kuua ushindani na kuwa na mnunuzi mmoja (Monopoly) Katika msimu wa kilimo wa 2024/2025 zao la pamba liliporomoka bei kutoka Tsh. 2,500 hadi Tsh. 1,200 na makato makubwa ya Tsh. 300 kwa kilo.

Mazao mengine yaliyoporomoka bei ni pamoja na choroko, dengu, mbaazi, ufuta kwa zaidi ya 50%. Pia mazao mengine kununuliwa kwa mkopo kama tumbaku na kugeuzwa mtaji wa wafanyabiashara bila ridhaa ya wakulima. Kwa dhuluma hizi wakulima hawahitaji kupewa pesa ili kuingia barabarani kudai haki yao.

(iv) Kuua masoko, ajira na viwanda vya ndani, baada ya kuua mifumo ya udhibiti na kuruhusu kuingia kiholela kwa bidhaa bandia, feki na zilizokwisha muda wa matumizi. Pia kuruhusu kuingia mazao na bidhaa zinazozalishwa kwa wingi nchini kama Sukari, Mafuta ya Kupikia, Mchele, Mbolea, Mbegu, Chanjo, Dawa za kuogesha mifugo nk. na hivyo kuua soko la ndani. Bidhaa hizo kutoka nje ya nchi husamehewa kodi wakati bidhaa za ndani zinatozwa kodi kubwa na hivyo kuua ushindani.

Hivi sasa soko la mchele nchini limeanguka kutokana na kuingia kwa wingi mchele kutoka nje ya nchi, kashfa ya uingizaji wa sukari kiholela ya mwaka 2024 ilipelekea wakulima wa miwa na viwanda vya ndani vya sukari kukosa soko na taifa kupata hasara ya zaidi Tsh. Trilioni 1.5.

Zabuni na kandarasi kupewa wageni hata kwa kazi ambazo wanaweza kufanya watanzania na mbaya zaidi wazawa hawalipwi madeni ambayo yamefikia zaidi ya Tsh. Trilioni 7.8 hali iliyowafanya wafilisike na ajira kupotea. Pia wazawa wamekuwa hawashirikishwi kikamilifu katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali.

(v) Misamaha ya kodi inatolewa kwa upendeleo hasa kwa Makampuni ya nje (Wawekezaji mahiri) huku adhabu za ukwepaji kodi zikitolewa kwa wazawa pekee. Mfano Makampuni makubwa ya kimataifa MNCs yamesamehewa adhabu ya 100% kwa miamala ya

kukwepa kodi ya Transfer Pricing, Pia utitiri wa tozo, ushuru, ada na kodi hutozwa kwa wazawa hali inayopelekea kuelemewa na kufunga biashara na kusababisha kuua ajira.

(vi) Kushamiri kwa uvuvi haramu, madawa ya kulevya, maeneo ya wachimbaji wadogo kupewa wageni, utoroshaji mkubwa wa raslimali kama madini, mazao ya uvuvi na mifugo nk.

2.3 Masuala ya Kijamii yanayojumuishwa mmomonyoko wa maadili na kushuka kwa uzalendo, kutopatiwa ufumbuzi na majibu stahiki yamekuwa kero katika jamii kama vile, Rushwa, Ubadhirifu wa mali za umma na madai ya utekaji na kupotea kwa watu.

Rushwa na ubadhirifu wa mali za umma, taarifa za CAG, PPRA, FIU, PCCB, IAG zimekuwa zikiripoti upotevu mkubwa wa matrilioni ya fedha za umma kila mwaka. Wabunge na wananchi wamelalamikia ufisadi uliokithiri serikalini katika kipindi cha miaka 5 iliyopita bila mafanikio yoyote huku wezi wa fedha na raslimali za umma wakiruhusiwa kula kwa urefu wa kamba, mara wezi watajwe kwa majina waone aibu na wengine kupewa zawadi ya teuzi katika vyombo vya maamuzi kama ubunge, uwaziri mpaka uwaziri Mkuu badala ya kufikishwa mahakamani. Ipo mifano mingi:-

(a) Kuna tuhuma za wizi wa kutisha kwenye mikopo ya Serikali ambapo kwa miaka 5 iliyopita deni la Serikali limeongezeka kutoka Tsh Trilioni 60.9 Machi 2021 hadi Tsh. Trilioni 115.2 Februari 2026 sawa na ongezeko la Tsh. Trilioni 54.3. Deni

limeongezeka kutoka ukuaji wa 7% hadi 19% hii kasi ya ongezeko sio la kawaida (Skyrocketting debt).

Kwa sehemu kubwa mikopo imechukuliwa kwa siri na nje ya bajeti, matumizi yake hayafahamiki na fedha nyingine zimepita kwenye akaunti za watu binafsi badala ya mfuko mkuu wa Serikali kinyume na Ibara ya 135 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 12 cha Sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348 na marekebisho yake ya mwaka 2020.

(b) Kuwepo kwa mianya na mifumo ya kodi inayoruhusu fedha za umma kuingia kwenye mifuko ya watu binafsi na kupoteza mapato ya Serikali zaidi ya Tsh. Trilioni 40 kila mwaka.

(c) Tuhuma za wizi wa kutisha katika mradi wa SGR ambapo Serikali ilikiuka sheria ya Manunuzi na kuongeza gharama za mradi kwa zaidi ya Tsh. Trilioni 3.4 kwa lengo la kufuja fedha za umma huku ujenzi wa SGR Lot 3, Lot 4, Lot 5 na Lot 6 ukiwa umetelekezwa.

(d) Tuhuma za wizi wa kutisha katika mikataba ya kifisadi ya ujenzi wa barabara za lami kupitia utaratibu wa EPC+F wa Tsh. Trilioni 3.75

(e) Tuhuma za malipo ya fidia hewa katika Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji na Biashara (ICSID) na kupoteza fedha

za umma zaidi ya Tsh. Trilioni 2 katika kipindi cha miaka 5.

Kesi nyingi za mchongo za raslimali zinazidi kufunguliwa na kuamuliwa ili kuhalalisha wizi wa fedha za umma katika Mahakama za nje wakati Kifungu cha 11 cha Sheria ya Natural Wealth and Resources (Permarnent Sovereignty) Act 2017 ambayo inakataza kutumia Mahakama za nje ya nchi (Foreign Courts) katika mashauri yote yanayohusu raslimali za nchi. Fedha hizi zimekuwa zikilipwa kwa siri na bila ridhaa ya wananchi kinyume na misingi ya uwazi na uwajibikaji.

(f) Tuhuma za wizi wa kutisha katika Mradi wa Bwawa la kufua umeme ya Julius Nyerere (JNHPP-2115) ambapo zaidi ya Tsh. Trilioni 2.418 zimetafunwa na ubora wa mradi ni wa kutiliwa mashaka. Gharama za mradi zimeongezeka kwa Tsh. Bilioni 940 kutoka Tsh. Trilioni 6.5 hadi Tsh. Trilioni 7.44 bila sababu za msingi, mashauri hewa ya usuluhishi ISCID yamelipwa kiasi cha Tsh. Bilioni 889.6, kutokutekelezwa miradi ya Kijamii (CSR) ya Tsh. Bilioni 262 na kutokukata faini ya ucheleweshaji wa mradi ya Tsh. Bilioni 327.

(g) Kashfa kubwa ya kuiba fedha za wastaafu katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PSSSF kwa kisingizio cha kujenga uwanja wa ndege wa Serengeti (Serengeti Airport) wenye gharama ya Tsh. Bilioni 362.47.

Bodi ya PSSSF ilivunjwa baada ya kugoma kuidhinisha fedha za ujenzi wa uwanja huo tarehe 24 Aprili 2026 na baada ya siku 20 ilipofika tarehe 14 Mei 2026 Bodi hiyo ilivunjwa lakini Mkurugenzi Mkuu (DG) akiachwa aendelee na majukumu yake.

Ziko taarifa kuwa Bodi ya PSSSF ilibaini tathmini ya mradi haikufanyika kikamilifu kwani mradi huo hauwezi kurejesha fedha kwa wakati na hivyo kuathiri ukwasi wa mfuko kuhudumia wastaafu. Sababu zingine ni mfuko kuwa na miradi mingi ambayo haifanyi vizuri na imeshindwa kurejesha fedha za mfuko kwa wakati (Stalled and White elephant projects).

Miradi mingi haijakamilika ukiwemo Mradi wa kumbi za mikutano AICC Arusha wa zaidi ya Tsh. Bilioni 350. Mfuko unadaiwa madeni makubwa ya kodi na TRA ya takriban Tsh. Bilioni 800 hivyo kwa namna yoyote mfuko unapaswa kuelekeza nguvu katika kufufua na kukamilisha miradi inayoendelea badala ya kuanzisha mradi mwingine mpya. Hata hivyo nini lengo la kujenga uwanja wa Serengeti wakati ujenzi wa uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwanza unasuasua na haujakamilika hadi leo kwa zaidi ya miaka 5 sasa.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF anatuhumiwa kuiondoa Menejimenti akiwemo Mkurugenzi wa Uendeshaji (DO), Meneja wa Uwekezaji (IM),

Meneja wa Sheria (LM) na Mkurugenzi wa Fedha (DF) bila idhini ya Bodi ya Wadhamini.

Wastaafu wa nchi yetu wanapitia kipindi kigumu mara baada ya kustaafu kutokana na kucheleweshewa mafao na makato makubwa yasiyo na sababu za msingi ikiwemo kuanzisha kikotoo kipya na kuwapunja wastaafu. Hii inatokana na Serikali kushindwa kusimamia fedha za mifuko ya hifadhi za jamii na kuruhusu wizi na udanganyifu kutapanya fedha za wastaafu.

(h) Tuhuma ya kashfa ya uingizaji wa Sukari kiholela ndani ya nchi ambapo nchi ilipoteza zaidi ya Tsh. Trilioni 1.5 huku wakulima wa miwa na viwanda vya ndani vikikosa soko.

(i) Tuhuma za wizi wa kutisha katika uagizaji na usambazaji wa mafuta ya Dizeli na Petroli kutokana na kuruhusu upandishaji wa bei kiholela na kuwaibia wananchi matrilioni ya fedha kila mwezi.

(j) Tuhuma za wizi wa kutisha katika uagizaji kutoka nje na usambazaji wa mbolea ya ruzuku ambapo zaidi ya Tsh. Trilioni 1 katika kipindi cha miaka 5 zimepotea.

(k) Tuhuma za kukithiri kwa utakatishaji wa fedha haramu hadi nchi yetu kuingia kwenye orodha ya nchi oevu za utakatishaji wa fedha haramu duniani, pia miamala shuku (suspicious

transaction) imeongezeka mara dufu kutoka Tsh. Trilioni 122 mwaka 2022, Tsh Trilioni 280 mwaka 2023 hadi kufikia Tsh. Trilioni 463 mwaka 2024 huku taarifa za miamala fiche (Hidden Transaction) zikifichwa kwa nguvu kubwa. Utoroshaji wa fedha nje ya nchi umeongezeka (Illicit Financial Flows) na hakuna mtu anayechukuliwa hatua wala kuwajibika kwa kuwa mtandao huo unahusisha baadhi ya Viongozi waandamizi wa Serikali (Serious Organized Crime-SOC).

Mnamo mwezi Februari 2026 tumeshuhudia meli yenye shehena kubwa ya dawa za kulevya iliyokuwa inapeperusha bendera ya Tanzania ikikamatwa nchini El Salvado ikiwa na tani 6.6 za dawa za kulevya aina ya Kokeini.

(l) Kashfa ya wizi wa kutisha katika Mkataba ya Uendeshaji wa Bandari ya Dar es Saalaam ambapo mkataba wa IGA ambao una kila aina ya udanganyifu na harufu ya rushwa uliingiwa licha ya kukataliwa na watanzania walio wengi. Mikataba 3 ya HGA’s imeingiwa kwa siri na bila ridhaa ya Bunge ambapo tarehe 15 Aprili 2024 Serikali ilikabidhi Uendeshaji wa Bandari katika Gati namba 1 hadi Gati namba 7 kwa Kampuni ya DP World ya Dubai kwa muda wa miaka 30. Nguvu kubwa iliyotumika ililenga kumilikisha mali

za umma kwa watu binafsi na kwa manufaa binafsi.

Kampuni ya DP World licha ya kupewa kiwango kidogo cha kuwekeza cha Tsh. Bilioni 675 tu kwa kipindi cha miaka 5 lakini imeruhusiwa kupata 40% ya mapato yote katika gati namba 1 hadi gati namba 7.

Ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam ikiwemo kupunguza siku za kutoa mzigo, kuongeza mapato, kutia nanga meli kubwa na ndefu, uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA unatokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya awamu ya Tano kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa DMGP wenye thamani ya zaidi ya Tsh. Trilioni 1.118 katika bandari ya Dar es Salaam. Pia uboreshaji uliofanyika bandari ya Tanga na siyo ujio wa DP World kama inavyopotosha na Viongozi wa Serikali.

Aidha Serikali ya awamu ya 6 imeingia mikataba mingi mibovu na ya siri, bila ushindani na bila ridhaa ya Bunge ikiwemo mikataba ya raslimali 43 na ya Ubia 74 baadhi ya mikataba ni kama ifuatavyo:- Mkataba wa TPA na Adani Group, Nguala Rare Earth Project, Uwanja wa Ndege wa KIA, Ngorongoro, TFS, Vitalu vya Uwindaji, Liganga na Mchuchuma, NHC, STAMICO, DART,

TANROADS (Barabara ya njia 8 ya kulipia kutoka Kibaha hadi Chalinze), Makaa ya Mawe nk.

Serikali ya awamu ya 6 imevunja Kifungu cha 12 cha Sheria ya ulinzi wa raslimali (The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty) Act No. 5 of 2017) Cap 449 inayotaka mikataba ya raslimali kupelekwa Bungeni na kuridhiwa kabla ya kuanza utekelezaji na Sheria ya TEITA inayotaka uwazi katika michakato ya Manunuzi katika miradi ya raslimali. Pia kitendo hicho ni kinyume na UN Economic Charted on Natural Wealth and Sovereignty.

Baadhi ya Viongozi wa Umma (Political and business elites) wamekuwa wakituhumiwa kuwa na utajiri usioelezeka kumiliki akaunti za fedha nyingi Ughaibuni, kumiliki mabasi, Malori, vituo vya mafuta, mahoteli, Maduka makubwa na Super Market, viwanda, magorofa, mahekalu katika maeneo mbalimbali nchini na nchi za ughaibuni kama Dubai, South Africa, Uturuki, Ubelgiji nk. huku wananchi wengi wakiwa kwenye lindi kubwa la umasikini.

Orodha ya watuhumiwa wa wizi, rushwa, ufisadi na ubadhirifu wa fedha na raslimali za umma ni ndefu sana lakini kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, Rais na aliyekuwa Waziri wa Fedha (Waziri Mkuu wa sasa) ni watuhumiwa wa kwanza.

Nchi nyingine duniani ulimbikizaji wa mali za umma kwa watu wachache binafsi hatua kali huchukuliwa dhidi yao ikiwemo kutaifishwa mali na fedha, kufungwa gerezani na wengine

kunyongwa hadi kufa. Mfano wa hivi karibuni Mahakama ya kijeshi nchini China mnamo tarehe 7 Mei 2026 iliwahukumu adhabu ya kifo Mawaziri wawili wa Ulinzi, **Wei Fenghe na Li Shangfu** baada ya kupatikana na hatia ya makosa ya kupokea rushwa kubwa, kukiuka taratibu za manunuzi na matumizi mabaya ya madaraka. Lakini kwa bahati mbaya hapa nchini kwetu Viongozi wa aina hiyo hupewa kinga, heshima na kuzawadiwa vyeo na teuzi. Wananchi wanaofanyiwa haya yote hawawezi kuendelea kubaki kimya kwa kuhofia ***Mikwaju*** *y*a mtawala***.**

Utekaji, kupotezwa na kuuawa ni tatizo lililoshamiri nchini mwetu, watu wengi wamepotea na wengine kuuawa. Kwa mujibu wa Ripoti ya Tume ya Jaji Chande, jumla ya watu waliotekwa na kupotea ni 758 huku kati yao watu 245 waliopotea mwaka 2023 hadi 2025 hawajapatikana hadi leo. Pamoja na ukubwa wa tatizo na wingi wa matukio hayo Serikali imekuwa haitoi taarifa kikamilifu wala kufanya jitihada ya kudhibiti na kuwatafuta waliopotea. Ni Wajibu wa Serikali kulinda usalama wa raia hivyo matendo haya yanaifanya Serikali ikose sifa kikatiba.

Watu wengi wamekuwa wakikamatwa kwa kubambikiwa kesi na baadae kuachiliwa bila maelezo, mfano watu zaidi 1,651 waliokamatwa kwenye machafuko ya tarehe 29 Oktoba 2025 kwa makosa ya uhaini baadaye waliachiliwa huru kwa kile kilichoitwa msamaha wa Rais jambo ambalo halipo kisheria na ni ushahidi wa wazi kwamba walikamatwa na kushtakiwa kwa kuonewa. Jambo hili limelalamikiwa kwa muda mrefu pamoja na mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai lakini limekuwa likiendelea.

Tunakumbuka Mzee Ali Kibao wa CHADEMA alishushwa kwenye bus mchana kweupe Septemba 2024 na baadaye kwenda kuuawa na mpaka leo hakuna aliyeshtakiwa kwa kifo hicho. Huku baadhi ya wananchi na Viongozi wengine wa dini wakiamua kukimbilia uhamishoni nje ya nchi.

Kijana Shadrack Chaula aliyechora picha ya Rais Samia na baadaye kuichoma moto na watanzania kujitokeza kumlipia faini mahakamani baadaye alitekwa na kupotea Agosti 2024 na hajaonekana hadi leo.

Kama hiyo haitoshi, Padri Dk. Charles Kitima, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC) alivamiwa na watu wasiojulikana, alijeruhiwa vibaya na kunusurika kifo Mei 2025. Pia tulishuhudia kundi la watu linalojiita Wakatoliki wakitangaza kupeleka malalamiko kwa Baba Mtakatifu na kutishia kuitisha maandamano nchi nzima kupinga Viongozi wa Kanisa jambo ambalo lilionekana ni la kutengeneza na kuongeza uhasama lakini baadaye tukawaona Viongozi waandamizi wa Serikali wakiwa Vatican kwa Baba Mtakatifu Leo XIV.

Baadaye ikaelezwa na Rais hadharani Tarehe 2 Disemba 2025 alipokuwa anazungumza na aliowaita Wazee wa Dar es Salaam kwamba Serikali yake haifurahishwi na matamko ya kila mara yanayotolewa na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), ambapo matamko hayo 8 yalilaani matumizi mabaya ya raslimali za umma (Mkataba wa Bandari), utekaji, upotezwaji na mauaji ya raia wasio na hatia, machafuko ya Oktoba 2025 nk.

2.4 Utendaji usioridhisha wa baadhi ya watendaji na watumishi wa umma hususan ngazi za chini (Mamlaka za Serikali za Mitaa)

ikiwa ni pamoja na kutosikiliza au kutatua kero za wananchi kwa wakati na utekelezaji hafifu wa mapendekezo ya Tume mbalimbali zinazoundwa.

(i) Kero za wananchi, wananchi kuwa na kero za muda mrefu ambazo zimekosa ufumbuzi ikiwemo migogoro ya ardhi kila kona ya nchi, madai ya mirathi, mahusiano mabaya ya wananchi na wahifadhi, wananchi kutaifishwa mifugo yao, majanga ya moto ya kila mara, bidhaa feki, uchafuzi wa mazingira unaopelekea kuenea kwa magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) na yanayoambukiza (CDs) na kusababisha taifa kuwa na wagonjwa wengi na vifo. Ajali za barabarani ambapo kwa miaka 5 zaidi ya watu 7,636 wamekufa huku majeruhi wakiwa zaidi ya watu 12,663 nk.

(ii) Mapendekezo ya Tume zinazoundwa na Rais yamekuwa hayafanyiwi kazi, mfano Tume ya Haki Jinai, Tume ya Maboresho ya Kodi, Tume za Ngorongoro na haya ya Tume hii ya Matukio ya Oktoba 29, 2025, Kikosi kazi cha kukusanya Maoni ya wadau kuhusu uratibu Maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi, licha ya Taifa kutumia fedha nyingi kuzihudumia tume hizo mambo haya yanachochea hasira za wananchi.

2.5 Masuala yanayohusu uhusiano wa kimataifa katika dunia ya leo na ijayo ambapo mataifa mengi yanatanguliza mbele maslahi yao kama msingi wa mahusiano na kujaribu mbinu na mikakati mbalimbali ya kujiweka katika nafasi nzuri kuendeleza maslahi yao katika nchi nyingine, hasa zinazoendelea na zenye raslimali nyingi.

Nakubaliana na Tume kuwa mahusiano yetu na nchi nyingi Duniani yako kwenye hatihati kutokana kushamiri kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, kuminywa kwa demokrasia, kukandamizwa Uhuru wa Maoni na Vyombo vya Habari, utawala usiozingatia sheria na kuvunja itifaki na mikataba ya kimataifa.

Vile vile vikwazo vya uwekezaji ambapo kazi na miradi zinatolewa kwa upendeleo na rushwa, miradi kutolewa kwa usiri na bila ushindani kwa baadhi ya nchi fulani, kuwekewa masharti ya ziada yanayokinzana na Sheria za nchi. Pia mambo ya njoo kesho, njoo kesho kutwa ambayo yanapoteza muda mwingi na kuwakatisha tamaa na kushindwa kuwekeza nchini. Zipo baadhi ya nchi kubwa duniani kama Marekani zimeanza kufanya tathmini upya ya kina ya uhusiano wake na nchi yetu.

3. UHALALI WA VITENDO VYA SERIKALI WAKATI WA KUTULIZA GHASIA

3.1 Tume haikuchambua baadhi ya mambo muhimu ili kujiridhisha kama nguvu iliyotumika kukabiliana na waandamanaji ilikuwa sawa au laa!

(i) Tume ilipaswa kueleza kwa kina mazingira yaliyopelekea Jeshi la Polisi kuua watu zaidi ya 518, nani aliyetoa amri ya kuruhusu kuua na akina nani walihusika na mauaji hayo, kwanini risasi nyingi zilikuwa za kichwani, kifuani, tumboni na mgongoni.

(ii) Tume haijaonyesha uthibitisho wa Polisi kutumia mabomu ya machozi, maji ya washawasha, risasi za plastiki kama njia mbadala ya kukabiliana na waandamanaji.

(iii) Tume haijaeleza juu ya taarifa ya kuwepo kontena la silaha lililodaiwa kuingia nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam Agosti 2025 kipindi cha kuelekea uchaguzi Mkuu Oktoba 29, 2025.

(iv) Tume haijaeleza juu ya madai yaliyotolewa ya kuwepo askari kutoka nje ya nchi waliokuja kushiriki mauaji ya raia wasio na hatia.

(v) Tume haijaeleza madai ya baadhi ya askari waliovaa kininja na wengine kuvaa kiraia na kushiriki mauaji ya raia wasio na hatia, wengine wakiwa kwenye magari ya ya Polisi na ya kawaida.

(vi) Tume imeshindwa kueleza juu ya kauli ya aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mh George Boniface Simbachawene aliyoitoa tarehe 8 Disemba 2025 baada ghasia na machafuko ya uchaguzi mkuu kukemea na kulaani kitendo cha baadhi ya askari kuvaa kininja na kutumia nguvu kubwa kupitiliza katika udhibiti na ukamataji wa watuhumiwa. Mwezi mmoja baadaye Waziri Simbachawene alifukuzwa mnamo tarehe 8 Januari 2026 jambo ambalo lilipokelewa kwa hisia tofauti na wananchi kuwa ukamataji wa kikatili una baraka za mtawala angalia link hii https://youtu.be/1l9eLTwbqGM?si=fXbYk17v0_xt6Gvw

Yaliyomkuta Waziri Simbachawene yanafanana na yaliyomkuta aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi baada ya kukiri kuwa serikalini kuna matatizo makubwa katika majadiliano na kuingia

mikataba, kuna usiri mkubwa na matokeo yake nchi inaingia kwenye mikataba inayolinyonya taifa letu yenye masharti hasi na mingine ni tegesha kwa ajili ya kushtaki nchi kwenye Mahakama za Kimataifa za Usuluhishi wa migogoro ya biashara na uwekezaji (ICSID) na kuligharimu taifa letu kwa kiwango kikubwa. Profesa Kabudi aliyasema hayo tarehe 6 Disemba 2024 jijini Dodoma wakati akifungua kikao kazi cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali huku akitaka kiundwe chombo cha kuratibu na kusimamia mikataba nchini ili kukomesha michezo hiyo, katika hali ya kushangaza siku 2 baadaye ilipofika tarehe 8 Disemba 2024 Profesa Kabudi aliondolewa wizara hiyo. Angalia link http://youtu.be/ZKAittcZjeQ?si= LG3lwdD0w7qfXCl

Mfano mwingine wa hivi karibuni Bodi ya PSSSF imevunjwa baada ya kukataa kuidhinisha fedha za ujenzi wa uwanja wa ndege wa Serengeti mkoani Mara.

3.2 Tume imeshindwa kutoa taarifa sahihi ya watu waliopoteza maisha katika ghasia na maandamano ya tarehe 29 Oktoba 2025.

(i) Tume imeegemea taarifa za vifo zilizotolewa na vituo vya huduma za ya afya pekee na kuacha maeneo mengine muhimu ya Serikali za Mitaa na Vijiji na wenyeviti vitongoji kwani si maiti zote zilipelekwa hospitali ikizingatiwa kuwa kulikuwa na katazo la kutotoka nje.

Tume imeshindwa kutoa idadi halisi ya vifo kwani madai ya kuwa watu waliouawa wanaweza kuwa zaidi ya 518 ni sawa na kukubaliana na takwimu za watu wengine wanaosema kuwa watu waliouawa ni zaidi ya 10,000 katika mikoa na wilaya zilizokumbwa na machafuko.

(ii) Mchanganuo wa Tume katika ripoti yake ya idadi ya watu waliofariki katika Mkoa wa Dar es Salaam (182), Mkoa wa Mbeya (80), Mkoa wa Mwanza (90) na Mkoa wa Arusha (53), mchanganuo huo unaleta jumla ya watu 405 badala ya 518 hii ni tofauti ya marehemu 113. Makosa haya ya kitakwimu yanaleta mashaka kuwa takwimu hizo ni za kupika na zimechakachuliwa.

(iii) Pia Tume bila aibu imeficha idadi ya vifo katika Mikoa ya Shinyanga (Kahama), Geita (Geita na Katoro), Songwe (Momba &Tunduma), Mara (Bunda, Tarime) na Iringa ambapo taarifa zilizopo watu wengi waliuawa katika maeneo hayo.

3.3 Tume imeshindwa kuthibitisha madai ya mali iliyoharibiwa ya thamani ya Tsh. Bilioni 125 yakiwemo majengo ya CCM na Mahakama.

(i) Tume imeshindwa kuueleza umma chombo kilichofanya ukadiriaji na uthaminishaji wa mali zilizoharibiwa na kufikia hasara ya Tsh. Bilioni 125, hivyo madai haya hayana uthibitisho na pengine yamelenga kufuja fedha za umma kwa kisingizio cha fidia.

(ii) Tume imeweza kupata gharama za mali zilizoharibiwa lakini imeshindwa kukokotoa gharama za kifuta machozi za marehemu zaidi ya 518 na fidia, gharama za matibabu na vifaa saidizi kwa wananchi waliopata ulemavu wa kudumu zaidi ya 2,390.

(iii) Tume kwa siku zaidi ya 153 imeshindwa kukotoa madhara na hasara walizopata wananchi na taifa kwa ujumla kutokana na kuzimwa kwa Mtandao wa Intaneti na kuzuiwa watu kutoka ndani (Curfew na Lockdown) ambapo shughuli za kijamii na kiuchumi zilisimama kwa siku 6 mfululizo. Je zuio hilo lilikuwa na uhalali wa kisheria?

Kwa tathmini niliyofanya nchi ilipoteza zaidi ya **Tsh. Trilioni 5** ambapo Tsh. Trilioni 1 ni kodi ya Serikali na Tsh. Trilioni 4 ni mapato ya wananchi kutokana na shughuli zao za kiuchumi za kila siku kama biashara, mawasiliano, Benki, mikataba, uwekezaji nk.

Aidha madhara mengine ni pamoja na wananchi wengi walikosa huduma za afya na wengine kupoteza maisha kwa kukosa matibabu. Pia huduma za elimu, maji, chakula na huduma zingine muhimu ziliathiriwa na kuleta adha kubwa kwa wananchi.

3.4 Tume kushindwa kuthibitisha kauli za Viongozi (Rais na Waziri Mkuu) ambapo kwa nyakati tofauti walieleza umma kuwa watu walioshiriki maandamano hayo walitoka nje ya nchi, na wengi walifuata mkumbo, walipewa fedha kwanza ili waandamane na walifadhiliwa na taasisi za Nje na Ndani. Waziri Mkuu alidai kuwa

kuna mtu mmoja alipewa Tsh. Bilioni 5 ili azigawe kwa waandamanaji na akapiga marufuku kutaja idadi ya marehemu kwa kuwa kufanya hivyo ni sawa na kushangilia vifo.

(i) Tume imeshindwa kuthibitisha kama waandanamaji waliotoka nje ya nchi, walitoka nchi gani na namna walivyoingia nchini?

(ii) Tume imeshindwa kuweka wazi kuhusu nani aliyefadhili Tsh. Bilioni 5 na nani aliyezipokea, na ziligawiwa kwa utaratibu gani kwa waandamanaji.

(iii) Tume imetoa taarifa ya idadi ya waliouawa na kujeruhiwa kinyume na agizo la Waziri Mkuu lililozuia.

(iv) Tume imeorodhesha vyanzo vikuu vya maandamano na kupingana na Kauli ya Rais kuwa waandamanaji hawakuwa na ajenda mahsusi bali walilipwa na walifuata mkumbo.

Kushindwa kwa Tume ya Jaji Chande kuthibitisha ukweli wa kauli hizo au kubaini kinyume chake inaleta utata mkubwa kwa Viongozi hao kwenye jamii.

4. VITENDO VYA SERIKALI BAADA YA MATUKIO YA MAUAJI YA OKTOBA 2025

4.1 Vitendo vya Serikali baada ya matukio ya mauaji ya Oktoba 2025 vinadhihirisha wazi kuwa Serikali ina mgongano mkubwa wa maslahi kama ifuatavyo:-

(i) Serikali kuacha kutenga muda wa kuomboleza wala kupeperusha bendera nusu mlingoti katika kipindi cha

maombolezo kinyume na utaratibu wa siku zote nchi inapopata majanga ya kupoteza maisha ya watu wengi.

(ii) Madai ya baadhi ya majeruhi kuzuiwa kupewa huduma za matibabu na wengine kupelekwa mochwari wakiwa hai kwa amri ya polisi.

(iii) Madai ya Ndugu wa marehemu kunyimwa miili na hata walioruhusiwa kuchukua miili waliandikiwa kwenye vyeti vya kifo sababu nyingine na sio kuuawa kwa risasi.

(iv) Maeneo mengi yaliyokuwa makazi ya ombaomba na watu wenye matatizo ya akili hawapo huenda nao waliuawa wakati wa machafuko.

(v) Serikali kushindwa kufanyia kazi taarifa za kiusalama kutoka TCRA za terehe 17-26 Oktoba 2025 kuwa kulikuwa na mijadala katika moja ya mitandao ya Kijamii kuhusu namna watakavyotekeleza ghasia siku ya uchaguzi na kwamba kuna makundi yamejipanga kuharibu uchaguzi na yalikuwa yakiendesha mafunzo kwa vijana. Baadaye Tume ilibaini kuwepo nyumba waliyokuwa wakifanya mafunzo ambayo ilikuwa mita 10 kutoka kituo cha Polisi.

(vi) Tume imeshindwa kuchunguza sababu za kukamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya uhaini, ugaidi na ujambazi kwa vijana 1,651 na baadae kuachiliwa huru kwa kile kilichoitwa msamaha wa Rais.

4.2 Tume kushindwa kuchunguza matukio ya watu kutekwa, kupotea na kuuawa:

(i) Tume imepokea taarifa za Polisi pekee badala ya kuwahoji pia inaodai waliotekwa na baadaye wakapatikana watu 513. Pia Tume haijaeleza hatma ya watu 245 waliopotea ambao hawajapatikana hadi leo.

(ii) Tume imeamini taarifa ilizopewa na Polisi kuwa watu wengi wamepotea kwa sababu za mapenzi, ushirikana, madeni, kukwepa mkono sheria, huku ikijua wazi kuwa wapo wanasiasa wengi waliotekwa,kupotezwa kutokana na kuwa wakosoaji wakubwa wa Serikali, mfano Balozi Humphrey Polepole, Mchungaji Dkt. Godfrey Malisa, Mdude Nyagali, Deus Soka.

Baadhi yao kukimbilia uhamishoni kutokana na vitisho ili kunusuru maisha wakiweno Rose Mayemba, Sativa, Twaha Mwaipaya, Hilda Newton, Mchungaji Mbarikiwa Mwakipesile, Pastor Dickson Kabigumila na wengine wengi. Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) Agosti 2024 ilitoa orodha ya watu 83 waliotekwa na kupotea kutokana na misimamo yao ya kisiasa.

(iii) Tume imeshindwa kuhoji sababu za Polisi kushindwa kutangaza na kuchukua hatua dhidi ya watu au kikosi cha watu kinachohusika na utekaji, kupoteza na kuua raia wasio na hatia lakini badala yake imepokea simulizi kutoka Polisi ya idadi ya watu 758 waliotekwa na kupotea.

4.3 Tume kushindwa kutangaza gharama ilizotumia kufanya uchunguzi na Uhalali wa kuongezewa muda kutoka siku 90 hadi siku 153, hii ikiwa ni ziada ya siku 63 sawa na ongezeko la muda la 70%.

(i) Gharama zilizotumiwa na Tume hazikutangazwa hadharani kinyume na misingi ya utawala bora ya uwazi na uwajibikaji inavyotaka. Eneo hili lisipotazamwa kwa umakini linaweza kutumika kama uchochoro wa kufuja fedha na mali za umma.

(ii) Ongezeko la muda la ziku za ziada 63 za Tume kukamilisha kazi yake ni nyingi na Tume imeshindwa kuthibitisha Uhalali wa ongezeko hilo. Aidha Tangazo la Gazeti la Serikali (GN) la ongezeko la muda lilitolewa mwishoni na nje ya muda uliopaswa kuwasilisha ripoti ya Tume.

Tume ilipaswa kukamilisha kazi na kuwasilisha ripoti tarehe 20 Februari 2026 lakini GN ya ongezeko la muda ilitolewa siku hiyo hiyo iliyotakiwa kuwasilisha ripoti. Tume iliongezewa muda hadi tarehe 3 Aprili 2026 lakini GN ya kuongeza muda ilitolewa tarehe 4 Aprili 2026 nje ya muda wa kuwasilisha ripoti. Suala la kuongezewa muda haliwezi kufanywa kwa dharura ilipaswa walau siku 7 kabla ya siku ya kuwasilisha ripoti hivyo nyongeza ya muda wa siku 63 iliyoongezewa Tume haikuwa na sababu za msingi.

(iii) Ongezeko la muda lilitangazwa na Mwenyekiti wa Tume kupitia Press Release na GN badala ya Mamlaka ya

uteuzi hivyo kuleta mkanganyiko mkubwa kuhusu uhalali wa nyongeza ya muda wa kukamilisha kazi ya Tume.

Kutokana na mkanganyiko huo ni dhahiri kuwa Uhalali wa ongezeko la muda umeshindwa kuthibitika na pengine ulilenga kuwazubaisha wananchi na kuchakachua ripoti ili kuuficha ukweli na kufuja fedha za Umma.

4.4 Kupendekeza kuanzisha Tume nyingine ya jinai kuchunguza kwa kina na kubaini waliohusika katika matukio hayo ya mauaji ya Oktoba 29, 2025.

(i) Haitokei kuunda tume mbili kwa madhila yanayotokana na tukio moja au mnyororo wa matukio ambayo chimbuko lake ni moja tena chini ya mamlaka hiyo hiyo. Aidha jukumu kuu la Tume lilikuwa kubaini ukweli (Fact Findings) kuhusu matukio ya ghasia za wakati na baada ya uchaguzi Mkuu Oktoba 2025 na kwamba Tume iliundwa ikapewa Sekretarieti itakayoweza kufikia malengo hayo.

(ii) Pendekezo la kuunda tume nyingine chini ya Mamlaka hiyo hiyo ya Rais ni kuwapotezea muda wananchi, kufuja fedha za umma na ni ujanja wa kukwepa mchakato wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) na mamlaka zingine za kimataifa.

4.5 Kuzuia Ripoti ya Tume kupelekwa kwa wananchi na kudai ni mali ya Rais na isidaiwe na mtu yoyote.

(i) Awali wakati Mtawala anaunda Tume aliwaomba watanzania kuwa na subira wakati Tume inakamilisha kazi yake ili kulitoa Taifa hapa lilipo, baada ya ripoti kuwasilishwa nini kilibadilika hadi kuficha ripoti.

(ii) Kusoma muhtasari na kuzuia ripoti ya Tume kutodaiwa na mtu yoyote wala kwenda kwa Umma ni ishara kuwa maudhui yaliyowasilishwa kupitia muhtasari huenda yanakinzana na ripoti yenyewe na kwamba kuna mambo mengi yasiyo ya kawaida yanafichwa.

(iii) Ripoti ya Rais sio ya Siri hivyo kitendo cha Rais kukataa isiende kwenye Umma ni mwendelezo wa kuuficha ukweli ulioanishwa kwenye ripoti hiyo na kuthibitisha kwa uwazi mgongano mkubwa wa maslahi (Conflict of Interest)

(iv) Pia kuna mgongano wa ndani (Contradictions) ambapo Tume inaahidi wadau kusoma mapendekezo na Maoni ndani ya Ripoti kamili nanukuu ***"Nimetaja baadhi tu ya mapendekezo yaliyomo kwenye Ripoti, bila shaka wadau mbalimbali watapata fursa ya kuyasoma kwa kina ndani ya Ripoti"*** Mwisho wa kunukuu (Uk.58 wa Hotuba ya Mwenyekiti wa Tume) lakini Rais baada ya kupokea

ripoti hiyo alisema ni Ripoti yake na haipaswi kudaiwa na yeyote.

Jambo la kushangaza zaidi Tume ya Jaji Chande ilipopata fursa ya kutoa Ufafanuzi kwa waandishi wa habari Tarehe 28 Aprili 2026, Dar es Salaam kuhusiana na Ripoti yao waliyokabidhi kwa Rais walisema ***"ripoti isingeweza kuwekwa hadharani kwa kuwa inajumuisha taarifa za siri"*** Kauli hii ni kinyume na tamko lao la kwanza siku wanakabidhi ripoti. Huu ni ushahidi wa wazi kuwa Tume hii haikuwa na msimamo kwenye jambo lolote na ilitegemea uelekeo wa mtawala pekee.

Kitendo cha kutoa ufafanuzi kwa umma hakikuwa na mantiki yoyote kwa kuwa Rais alishasema Ripoti hiyo ni yake na kwamba hata tume yenyewe ilikuwa imeshatamatika kisheria mnamo tarehe 23 Aprili 2026 baada ya kukabidhi Ripoti kwa Rais.

(v) Rais anadai kuwa ripoti ni mali yake binafsi na kama ni mali yake binafsi kwanini ametumia mali na fedha za umma kuhudumia tume hiyo kwa siku 153.

Marais waliotangulia tangu enzi ya Mwalimu Julius Nyerere ripoti zilitolewa na hata pale zilipowasilishwa kwa muhtasari taarifa zote muhimu ziliwekwa wazi ili umma uujue ukweli mfano Tume ya Jaji Kipenka (Mauaji ya Wafanyabiashara wa Madini Mahenge), Tume ya Jaji Warioba (Katiba Mpya), Tume ya Profesa Mruma (Makinikia) nk ambapo wahusika

walitajwa kwa majina na vyeo vyao na kuchukuliwa hatua za kiutawala na wengine kuburuzwa Mahakamani na kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa.

(vi) Tume imepata hofu na kuogopa kuishutumu Serikali (Inferiority Complex) kutokana na uhusika wake katika machafuko ya Oktoba 29, 2025. Tume imeshindwa kutafiti na kufanya uchunguzi wa mambo muhimu, imekuwa na kigugumizi kueleza ukweli lakini pia imekiuka kwa makusudi Sheria na Kanuni za kufanya uchunguzi na utafiti na kubakiza simulizi.

(vii) Serikali kutoa taarifa kwa umma ni jambo la lazima na siyo hiari, Raia wa Tanzania wanayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii na kudai uwazi na uwajibikaji. Hii pia ni kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 4 cha Sheria ya upatikanaji wa taarifa kwa umma (Access to Information Act).

5. UHALALI WA MAANDAMANO YA OKTOBA 2025

Tume katika hitimisho lake kuhusu uhalali wa maandamano ya Oktoba 2025 ilidai kuwa hayakuwa maandamano ya amani bali yalikuwa ni matukio ya ghasia zilizoambatana na matukio ya uvunjifu wa amani, Tume ilibainisha kwamba waandamanaji walikuwa nje ya kinga iliyowekwa kitaifa na kimataifa na hivyo uvunjifu huo ulisababisha Serikali kutumia nguvu kubwa

kukabiliana na waandamanaji hao. Hitimisho hilo la Tume halitendi haki kwa waandamanaji kwa uchambuzi ufuatao:-

(I) Madai ya kuwa Waandamanaji hawakutoa taarifa polisi

Ukweli ni kwamba kabla ya siku ya uchaguzi, vuguvugu la maandamano lilienea kila kona ya nchi ambapo Rais, Waziri wa Mambo ya ndani na Jeshi la Polisi walionya na kupiga marufuku maandamano kuelekea siku ya uchaguzi mkuu badala ya kujipa muda wa kusikiliza madai ya wananchi. Wahusika hao mara kwa mara walitoa vitisho na hivyo isingekuwa rahisi kupelekewa notisi.

Imani ya wananchi kwa Jeshi la Polisi imepungua kutokana na jeshi hilo kushindwa kudhibiti matukio ya uhalifu kama utekaji, upotezwaji na mauaji yanayofanyika kila kona ya nchi na hivyo wasingeona kama ni chombo halali cha kukimbilia.

(II) Madai ya kwamba eti Waandamanaji walizuia haki ya mpiga kura

Kwa kifupi hapakuwa na uchaguzi Oktoba 29, 2025 bali kulikuwa na mapinduzi ya Kiraia (Civilian coup) kujiweka kwenye uongozi kwa njia ya udanganyifu na mtutu wa bunduki badala ya kuchaguliwa na wananchi, kujiweka madarakani kwa udikteta badala ya njia ya kidemokrasia na hivyo Rais, Wabunge na Madiwani wamepatikana kwa njia zisizo halali, kinyume cha Sheria na Katiba ya Nchi. Hivyo maandamano yalilenga kudhibiti uharamia huo uliolenga kupoka haki ya raia kuchagua viongozi wanaowataka.

Uchaguzi wa mwaka 2025 hata waangalizi wa Jumuiya za SADC, AU waliukataa kwamba haukuwa huru, haki wala wa kuaminika

na kwamba ulikuwa na dosari nyingi kiasi cha kutokukidhi viwango vya demokrasia na hata baadhi ya Jumuiya za Kimataifa zimetaka uchaguzi urudiwe kwa kuwa uchaguzi uliofanyika haukuwa huru, haki wala wa kuaminika. Baadhi ya changamoto ni kama ifuatavyo:-

Upande wa CCM.

(a) Uteuzi wa mgombea wa urais wa CCM, Ndg. Samia Suluhu Hassan ulipingwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa na mwanachama mwenzake wa CCM kutoka Kwimba, Mwanza, Ndugu Devidlevi Nestory Nkindikwa. Pia mwanachama mwingine wa CCM wa Moshi, Kilimanjaro Mchungaji Dkt. Godfrey Malisa alipinga uteuzi huo Mahakama Kuu ya Tanzania kwa madai kuwa mgombea huyo hakuwa amechukua fomu, Mkutano uliompitisha haukuwa na ajenda ya uchaguzi, hakujaza fomu, jina lake halikupita kwenye vikao vya mchujo huku mgombea huyo akiendesha yeye mwenyewe vikao vya uteuzi wake jambo ambalo ni kinyume na Kanuni na Katiba za CCM na Sheria ya Vyama vya Siasa kifungu cha 4 (5) (b), 6 A (2) Sura ya 258 RE 2019.

(b) Tarehe 26 Agosti 2025, Msajili wa Vyama vya Siasa alitoa uamuzi wa malalamiko ya Ndugu Nkindikwa kwamba hawezi kushughulikia malalamiko hayo kwa kuwa suala la uteuzi wa mgombea wa CCM liko Mahakama Kuu jambo ambalo lilikuwa ni la uongo kwani Mahakama Kuu ilikuwa imeshaifuta kesi hiyo tangu tarehe 22 Agosti 2025. Uamuzi wa Msajili ulilenga kumlinda mgombea wa CCM asienguliwe kugombea na Tume ya Uchaguzi.

(c) Mchungaji Dkt. Malisa baada ya kesi yake ya kupinga uteuzi wa Samia kutupwa na Mahakama Kuu alikata rufaa Mahakama ya

Rufaa Tanzania Oktoba 6, 2025 ambapo kesi yake ilipakiwa hadi uchaguzi kupita na bado mpaka leo haijasikilizwa na kibaya zaidi alitekwa na watu wasiojulikana na baadaye kufunguliwa kesi ya Uhaini Januari 2026 na kusota gerezani hadi tarehe 19 Mei 2026 alipoachiwa huru na kufutiwa mashtaka.

(d) Balozi Polepole ambaye naye alipinga mchakato wa kumpitisha mgombea wa CCM kwa kueleza kuwa kikao hicho hakikuwa na ajenda ya uchaguzi na kusisitiza kuwa 'Samia Must Go' ambapo muda mfupi baada ya kauli hizo alitekwa na watu wasiojulikana na hadi sasa ni miezi zaidi ya 8 hajulikani alipo.

Pia Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima alipoibua hoja ya watu kutekwa na kupotezwa na kudai uwajibikaji, vikao vya uchujaji majina ngazi zote vilielekezwa kutopendekeza majina ya watu aina ya Gwajima *(Magwajimanization)* na baadae akapoteza nafasi ya kugombea huku Kanisa lake la Ufufuo na Uzima lenye matawi zaidi 2000 kote nchini likafungiwa na kuwazuia waumini kuabudu kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu.

Pia idadi kubwa ya Madiwani na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi waliokuwa wakidai uwazi na uwajibikaji wa Serikali walikatwa majina katika hatua za awali ili wasipate fursa ya kugombea na kuchaguliwa na wananchi jambo hili lilileta manung'uiko makubwa kwa wanachama wa CCM na wananchi nchi nzima.

Upande wa ACT Wazalendo

(i) Baada ya mimi Luhaga Joelson Mpina kuchaguliwa kihalali na Mkutano Mkuu wa Chama cha ACT

Wazalendo kupeperusha bendera kwa nafasi ya Rais Nilizuiwa kurejesha fomu wala kufika ofisi za INEC Agosti 27, 2025 kwa madai kuwa Msajili wa Vyama vya siasa amefuta uteuzi wangu, hii ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, Mgombea wa nafasi ya Urais aliyezunguka nchi nzima kutafuta wadhamini, kula kiapo Mahakama Kuu na kulipia Tsh. Milioni 1 ya fomu kuzuiliwa kurejesha fomu na bila hata kupewa nafasi ya kusikilizwa jambo ambalo lilikuwa kinyume cha Sheria ya uchaguzi na Katiba ya Nchi.

(ii) Hata pale Mahakama Kuu iliponipa ushindi na kuamua nirejeshe fomu na uteuzi uendelee bado Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndg. Hamza Said Johari aliniwekea pingamizi akirejea maamuzi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, pamoja na kutoa utetezi kuwa kwamba uamuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa nimeupinga Mahakama Kuu kwa shauri Na. 23438 ya mwaka 2025 chini Mheshimiwa Jaji Wilbert Chuma hivyo maamuzi hayo hayawezi kutumika tena kwenye pingamizi hadi hapo Mahakama itakapoamua vinginevyo. Pamoja na utetezi huo wa kisheria na kikatiba bado INEC ilikubaliana na pingamizi la AG na kuniondoa kwenye orodha ya wagombea.

(iii) Hata baada ya kufungua shauri lingine Mahakama Kuu na baadaye Mahakama ya Rufaa tarehe 22 Oktoba 2025 kwa shauri Na. 2122 la mwaka 2025 shauri hilo halikusikilizwa hadi uchaguzi kufanyika na mpaka leo licha ya kufanyika Kikao cha kiutawala kilihusisha pande

mbili za waleta rufaa (Mimi na Chama cha ACT Wazalendo) na Wajibu rufaa (Hamza Said Johari (AG) na Dkt Ally Possi (SG) na Wakili wa Serikali Mark Mulwambo chini ya Uenyekiti wa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa George Masaju. Isingetarajiwa kwa nchi inayofuata misingi ya Sheria na demokrasia kuendelea na uchaguzi huku mmoja wa mgombea ana kesi Mahakamani ya kupinga kuenguliwa kwake.

Kushindwa kuamuliwa kwa kesi hiyo kulipelekea Chama cha ACT Wazalendo kukosa Mgombea Urais na Makamu wa Rais **Bi Fatma Abdulhabib Ferej**, Hata hivyo nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mawakili waliosimamia kesi zangu za uchaguzi katika hatua zote Wakili Msomi Omar Said Shaaban (Mwanasheria Mkuu wa Chama), Wakili Msomi John Seka, Wakili Msomi Edson Kilatu na Wakili Msomi Jasper Sabuni na kwamba mapambano bado yanaendelea.

(iv) Vyombo vya Serikali vya INEC, RPP na AG vinatumika kama silaha ya kuwaengua wagombea wa upinzani ili kuua ushindani na kuwafanya wagombea wa CCM wa nafasi ya Rais, Ubunge na Udiwani kupita bila kupingwa.

Mfano Kesi ya Mwana CCM, Nkindikwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa alijibiwa kuwa Msajili hatashughulikia suala ambalo liko Mahakamani na anabanwa na Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini upande wangu niliienguliwa na INEC licha ya kueleza kuwa pingamizi la Mwanasheria Mkuu

wa Serikali limepingwa Mahakamani. Hii ni *double standard* na upendeleo uliopitiliza.

(v) Chama cha ACT Wazalendo kunyimwa nafasi ya Viti Maalum katika nafasi za ubunge na udiwani licha ya kupata 6.677% ya kura zote za wabunge ambapo ilistahili kupata viti zaidi ya 6 vya ubunge huku chama cha Chauma kikipewa viti 2 kinyume na Ibara ya 78 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Upande wa CHADEMA

(i) Tundu Lissu, Mwenyekiti wa CHADEMA alikamatwa na kufunguliwa kesi ya uhaini Aprili 2025 na chama chake kilifungiwa kufanya shughuli za kisiasa kwa kupitia Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Mstaafu Fransis Mutungi na baadaye Mahakama Kuu hivyo chama hicho kilizuiwa kufanya shughuli za kisiasa kwa mwaka mzima na kimekuja kufunguliwa tena Aprili 2026 baada ya uchaguzi kumalizika.

Nakumbuka siku nilipokwenda Mahakamani kuhudhuria kesi yake alifurahi sana huku akisema Mpina kaza, kaza kabisa be strong, nami nilimwambia najua uko jela kwa tuhuma za uongo lakini yana mwisho haya.

(ii) Uamuzi wa zuio la kukifungia chama cha CHADEMA uliotolewa chini ya Jaji Hamidu Mwanga umekuja kufutwa na Mahakama ya Rufaa Aprili 16, 2026 huu ni ushahidi wa wazi kuwa chama hicho kilionewa ili

kisishiriki katika kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu wa 2025.

(iii) Pia viongozi wengi wa CHADEMA walikamatwa kwa kusingiziwa makosa mbalimbali na wengine kulazimika kukimbilia nje ya nchi.

Mazingira ya Uchaguzi

Zilijitokeza dosari nyingi katika zoezi la uandikishaji wapiga kura, kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo na hata Uhalali wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Tume ya uchaguzi iliteuliwa na Rais ambapo ameteua wajumbe bila ushindani na kwa upendeleo wa hali ya juu kwa misingi ya Ndugu, jamaa na marafiki kama ifuatavyo:- Jaji Jacobs Mwambegele (Mwenyekiti), Jaji Mbarouk Salim Mbarouk (Makamu), Wajumbe wengine ni Jaji Asina A. Omari, Balozi Omary Ramadhani Mapuri, Dkt. Zakia Mohamed Aboubakar, Magdalena Kamugisha, na Ramadhani Kailima (Katibu na Mkurugenzi wa Uchaguzi).

Tume hii iliteuliwa mwaka 2023 wakati huo ikiitwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na hivyo muda wake kisheria ulitamatishwa mara baada ya Sheria na jina la Tume kubadilishwa mwaka 2024 na kuwa Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) waliruhusiwa kusimamia uchaguzi wakiwa hawana sifa kisheria na kinyume na Kifungu cha 5 (1) (2) (a) na (b) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2024 ambayo inataka wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi wapatikane kwa njia ya ushindani kwa kuomba nafasi hizo na kufanyiwa usaili.

Hivyo uchaguzi wa mwaka 2025 ulisimamiwa na Tume batili ambayo haina mamlaka kisheria ni sawa na kusema uchaguzi huo ulisimamiwa na genge la mtu binafsi. Dosari zingine ni kama ifuatavyo:-

(i) Mawakala wengi wa ACT Wazalendo walizuiwa kuingia katika vituo vya kupigia kura na hivyo kushindwa kushiriki zoezi la upigaji kura, kuhesabu, majumuisho ya kura na kutangaza matokeo.

(ii) Baadhi ya masanduku ya kura yaliondoka na magari ya polisi na kwenda kusikojulikana, baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi walionekana wakitiki karatasi za kupigia kura na baadhi ya vituo walionekana watu wakitumbukiza lundo la karatasi za kura za Rais, Wabunge na Madiwani.

(iii) Mawakala wengi hawakupewa fomu za majumuisho ya kura wala kusaini, wagombea na mawakala wengi wa ACT Wazalendo walikamatwa na kufunguliwa kesi za ugaidi, uhaini na ujambazi wakati zoezi la kupiga kura likiendelea. Wengine walipigwa hadi kuuawa mfano mgombea udiwani Kata ya Sirari, Tarime Mkoa Mara Dafroza K. Jacob.

(iv) Baadhi ya mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Arusha, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Songwe, Geita, Shinyanga na Mara jumla ya mikoa 11 na wilaya 21 kuliibuka machafuko makubwa ambapo baadhi ya vituo na maboksi ya kura yalichomwa moto, vurugu za maandamano na watu kuuawa lakini INEC iliwatangaza

wagombea wa CCM kwamba wameshinda kwa zaidi ya 95% maeneo hayo.

(v) Licha ya vituo vingi vya kura kuonyesha mwitikio mdogo wa wapiga kura kuwa kati ya 10%-23% lakini INEC ilitangaza mwitikio wa wapiga kura wa 87% na mgombea wa urais wa CCM kutangazwa mshindi 97.6%. Kwa maoni yangu, matokeo haya ni ya kughushi na hayana uhalisia.

(vi) Upande wa Zanzibar hali ilikuwa vilevile ya uingizaji wa karatasi za kura kwenye masanduku, karatasi za kura za kuzagaa mitaani, mawakala kutolewa vituoni na baadhi ya wagombea kuwekwa kuzuizini na kupigwa na kuumizwa vibaya na huku vyombo vya dola vikitoa vitisho vingi, kura hazikuhesabiwa wala kufanyiwa majumuisho. Hata kura za Rais wa Zanzibar hazikuhesabiwa wala kufanyiwa majumuisho ambapo hadi leo Mgombea wa Urais wa ACT Wazalendo, **Ndg. Othman Masoud Othman** hajapewa hati rasmi ya matokeo baada ya kunyang'anywa ushindi.

(vii) Licha ya takwa la kisheria la kuitaka INEC kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ndani ya siku 7 baada ya kutangaza matokeo leo ni zaidi ya miezi 7 imeshindwa kutangaza matokeo hayo.

(viii) Pia Jumuiya na Taasisi za Kimataifa wakiwemo waangalizi wa SADC, AU (AUEMO), Bunge la Ulaya (EU), Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu (UNCHR), walitoa taarifa zao kupinga

matokeo ya uchaguzi huo kwa kuwa unakinzana na Kanuni za uchaguzi wa kidemokrasia, huru, haki na wa kuaminika lakini pia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na kutaka uchunguzi huru ufanyike.

Tume Huru ya Uchaguzi kwa sehemu kubwa ndiyo lilipiga kura badala ya wananchi na kutangaza matokeo feki, hivyo kuandamana kwa wananchi walikuwa na sababu za msingi kwa kuwa huo haukuwa uchaguzi bali genge lililoamua kupindua mchakato wa kidemokrasia wa wananchi na kujiweka madarakani kwa nguvu (kidikteta).

(III) Madai ya kwamba Waandamanaji walikuwa na silaha (Bunduki)

(a) Tume imeibua tuhuma za kiujumla kwani siyo kweli kwamba waandamanaji wote walikuwa na silaha, pia imeshindwa kuweka ushahidi wa kuaminika. Mfano waandamanaji walikuwa na bunduki ngapi na za aina gani? Na je bunduki hizo zinamilikiwa kihalali au laa, na je walikamatwa waandamanaji wangapi wenye bunduki? Badala yake Tume imepiga simulizi tu. Hii sio sawa na ni dhihaka kubwa kwa taifa na kutowatendea haki marehemu kwa kuwa hawana uwezo wa kujitetea.

(b) Tume inaeleza kuwa walioshiriki maandamano ni wananchi wa kawaida na wengi wafuata mkumbo sasa kama ndivyo hivyo, wananchi hao walipata wapi silaha za bunduki hadi kutishia usalama wa nchi?

(c) Watu wote waliokamatwa kwenye vuguvugu la maandamano na kufikishwa Mahakamani kwa makosa ya

uhaini walisamehewa na haikuripotiwa kama baadhi yao walikutwa na silaha aina ya bunduki.

(IV) Madai ya kwamba Maandamano yalihatarisha usalama wa Taifa

Kwa kuwa Tume imeshindwa kuthibitisha kama waandamanaji walitumia silaha za moto na kuhatarisha usalama wa nchi ni dhahiri kuwa kilichoonekana kwa jamii ndio ukweli wenyewe kuwa waandamanaji hawakuwa na silaha (Unarmed protestors) na wengi wao waliuawa wakiwa wanakimbia kujisalimisha majumbani na wengine walikuwa barabarani, maeneo ya kahawa, kwenye vibanda vya kuangalia Mpira, visimani wakichota maji, madukani na sehemu zao za biashara (Picha na Video Clips zote zinaonyesha waandamanaji hawakuwa na bunduki). Hakuna picha wala video inayoonesha kuwepo majibizano ya risasi baina ya waandamanaji na Polisi. Zaidi askari walionekana wakiua kikatili watu wakubwa kwa wadogo waliokuwa wanakimbia ili kujiokoa.

Hapakuwa na vita wala hali ya hatari iliyokuwa imetangazwa na Rais kwa mujibu wa Ibara ya 32 (1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo maelezo ya tume kuwa waandamanaji walihatarisha usalama wa taifa hayana ukweli na msimamo wa Serikali kuwa ilibidi kutumia nguvu kubwa kupitiliza kuwadhibiti waandamanaji kurejesha amani na usalama wa nchi siyo ya kweli na hayana uthibitisho wowote.

Serikali imekiuka Sheria na mikataba ya kimataifa inayoweka ukomo wa kutumia nguvu kupitiliza (Necessary, Proportional and Reasonable force) kwani nguvu iliyotumika si ya busara haina

uwiano na kosa wala haikuwa na ulazima hii ni kinyume na Ibara ya 31 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, PGO na Sheria ya Matumizi ya Silaha na Risasi pamoja na mkataba wa African Charter on Human and People's Rights.

Haki za binadamu hazitekelezwi kwa utashi wa mtawala bali zinalindwa kisheria na mikataba ya kimataifa (International Human Rights Law, The United Nations Conventional on Civil and Political Rights of 1966 and The Universal Declaration on Human Rights 1948).

Mwandishi wa vitabu huko India, ***Radhakrishnan Pillai*** katika kitabu chake cha Corporate Chanakya alisema ni mwiko kwa kiongozi kutoa adhabu inayovuka mipaka ya sheria. Nanukuu ***"never ever try to do any serious injury that goes beyond the law"*** mwisho wa kunukuu.

Serikali ilivuka mipaka ya Katiba na Sheria kwa kutumia nguvu kupitiliza na kusababisha mauaji na ulemavu wa kudumu kwa raia wasio na hatia.

(V) Madai ya Waandamanaji walikuwa wafuata mkumbo

Maelezo ya Tume hayaeleweki na hayaaminiki kwa kuwa yana mkanganyiko mkubwa, awali Tume ilieleza kuwa wananchi wanazo sababu kuu 5 zilizopelekea kuwepo maandamano ambazo ndani yake kuna vipengele 20 na kwa kweli kwa uzito wa hoja hizo waandamanaji walikuwa na sababu za msingi za kuandamana na hivyo kitendo cha kuwatuhumu kuwa walifuata mkumbo ni madai ya uongo. Mashujaa hao walielewa fika wanachokifanya kuwa ni kulikomboa upya taifa lao.

5. MASUALA YA KIUCHUMI

Serikali ya awamu ya 6 iliruhusu rasmi wizi wa fedha na mali za umma ambapo watumishi wa umma waliambiwa wale kwa urefu wa kamba, watuhumiwa wa ufisadi kutangazwa kwa majina ili waone aibu badala ya kuchukuliwa hatua za kutumbuliwa na kufikishwa mahakamani, huku uzembe kwa watumishi wa umma nao ukapewa baraka hadi kufikia 40%.

Kama nchi tulipitisha Sheria mbili mwaka 2017 za kulinda raslimali za Taifa "*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act No. 5 of 2017 na The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act No. 6 of 2017*" Maamuzi na Mageuzi haya yalisisimua Afrika na dunia nzima kwa nchi ya Tanzania kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuzidisha mapambano ya ulinzi wa raslimali na fedha za Umma. Lakini leo hii Serikali ya awamu ya 6 inavunja sheria hizi kila uchao na hazisimamiwi tena.

Wizi huu mkubwa kupindukia unachelewesha mageuzi ya Kiuchumi na maendeleo, Taifa kuingia kwenye orodha ya nchi zenye mzigo mkubwa wa madeni (Heavily Indebted poor Country-HIPC).

Huku tofauti ya kipato kati ya wenye nacho na wasionacho ikizidi kuongezeka (Gini coefficient) takriban sehemu kubwa ya uchumi mkubwa wa nchi yetu unashikiliwa kundi la watu wachache na raia wa kigeni (Mafisadi wachache). Huku watumishi wa umma wakilipwa ujira mdogo usioendana na hali halisi ya ugumu wa maisha na hivi majuzi kwenye sherehe za **Mei Mosi 2026** watumishi wa umma wamenyimwa kuongezewa mshahara kwa

kisingizio cha fedha nyingi kutumika kwenye uchaguzi wa mwaka 2025 jambo ambalo haliwahusu na uchaguzi sio suala la dharura.

Katika uchaguzi wa mwaka 2025 tumeshuhudia ufuajaji mkubwa wa fedha za umma uliopitiliza ikiwemo Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kuwanunulia na kuwagawia wagombea wa urais magari mapya ya kifahari 19 kwa ajili ya kuendesha kampeni ya siku 60 kwa madai kuwa ni kuweka usawa katika kampeni (level playing field).

Huwezi kutumia fedha za umma zaidi ya Tsh. Bilioni 10 kununua magari 19 kwa kampeni za siku 60 wakati ungeweza kukodi magari kwa wagombea wote kwa fedha zisizozidi Tsh. Milioni 500 tu. Kama hiyo haitoshi hadi leo hakuna uthibitisho kama magari hayo yamerejeshwa serikalini, pia tulishuhudia Rais akibadilisha magari kwa sababu ya awamu yake ya kwanza imekwisha na sio magari hayo kuwa yamechakaa haya ni matumizi mabaya yaliyopitiliza ya fedha za umma.

Nikiwa mgombea wa Urais nilikataa gari hilo kwa kuwa niilijua ni matumizi mabaya ya fedha za umma, chanzo cha fedha hakikuwekwa wazi na kwamba kasma hiyo haikuwemo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Madai ya kuwa na uwanja sawa haikuwa na mantiki yoyote kwa kuwa INEC ilikuwa imeengua wagombea wengi wa upinzani kwa nafasi za Udiwani, Ubunge na Urais. Lakini pia suala la malipo ya mawakala liliachwa mikononi mwa wagombea na Vyama vyao hivyo suala la gari pekee haliwezi kuwa kigezo cha kuleta usawa katika uchaguzi bali ilikuwa ni mambo binafsi yaliyojificha nyuma ya pazia.

Hata kilichoelezwa na Tume ya Jaji Chande kuhusu kiwango cha nchi kuaminika katika kukopa kutokana na tathmini iliyofanywa na Kampuni ya Moody's na nchi yetu kupewa kiwango cha B1, watanzania tusiaminishwe na vigezo vya kampuni hiyo pekee kwani ukweli tunaujua kuhusu deni la Serikali ambapo vigezo vya uhimilivu vilivyowekwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) vya deni la Serikali vinakaribia kufikia ukomo uliowekwa (Thresholds or Borrowing ceilling limit).

Hadi kufikia Februari 2026 Deni la Serikali limeongezeka kwa Tsh. Trilioni 54.3 kiasi ambacho ni karibia sawa na Deni lote la nchi yetu la tangu Uhuru miaka 65 iliyopita lakini pia uwiano wa Deni la Serikali kwa pato la taifa (Debt-to GDP Ratio) umefikia 44% wakati ukomo ni 55% imebaki 11% tu kufikia ukomo. Uwiano wa ulipaji wa deni la Serikali kwa mauzo ya huduma na bidhaa nje (Debt Service to Export Ratio) umefikia ni 17% wakati ukomo ni 15-20%, hivyo tumeshavuka ukomo na ukomo wa mwisho tumebakiza 3%, uwiano wa ulipaji wa deni kwa mapato (Debt Service to Revenue Ratio) ni 14.5% wakati ukomo ni 18% hivyo tumebakiza 3.5% tu kufikia ukomo.

Pia Wafadhili wengi wamepunguza misaada na mikopo ya masharti nafuu na hivi sasa taifa limebebeshwa mzigo mkubwa wa riba kutokana na mikopo mikubwa ya Kibiashara (Commercial Debt Share) ambayo imefikia 35.8% kiwango hiki ni kikubwa kwani inatakiwa iwe chini ya 20%. Hatari nyingine ni kwamba takriban 70% ya deni hili liko kwenye Dola za Marekani na hivyo mtikisiko wowote wa kushuka thamani kwa Tanzania Shilingi dhidi ya Dola kunapelekea kuongezeka kwa deni la Serikali (High Forex and Currency Risks).

Tulipofanyiwa tathmini ya uhimilivu (Debt Sustainability Analysis) na **IMF, World Bank, *Tanzania Investment Centre and Consultant Group Limited-TICGL*** pamoja na maelezo kuwa deni ni himilivu lakini taasisi hizo zimetahadharisha kuwa nchi yetu iko kwenye hatari kubwa ya kuvuka viwango vya ukomo wa mikopo vilivyowekwa (High Vulnerability).

Huku deni la Serikali likiripotiwa kuongezeka kwa kasi isiyokuwa ya kawaida na fedha kutengwa kila mwaka lakini ni dhahiri kuwa zimekuwa bajeti hewa na fedha kutafunwa. Mfano ujenzi wa Reli ya SGR wa Lot 3 (Makutupora-Tabora) umefikia 14.53% na Lot 4 (Tabora-Isaka) umefikia 6.65% wakati mkataba hii yote ilipaswa kukamilika Disemba 2025. Mradi wa Lot 6 (Tabora-Kigoma) uko umefikia 7.88% wakati mkataba ulitakiwa kuwa umemalizika ifikapo Juni 2026, Lot 5 (Mwanza-Isaka) mradi umefikia 68.77% wakati mradi ulipaswa kumalizika Disemba 2024.

Kwa kifupi miradi ya SGR imetelekezwa katika kipindi chote cha miaka 5 licha ya Serikali kuripotiwa kukopa zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa kwenye bajeti na sasa inadai tena kupata mkopo mpya ya zaidi ya Trilioni 3.32 kwa ajili ya SGR. Swali la kujiuliza mikopo ya nyuma imeenda wapi iliyokuwa ikichukuliwa kwa zaidi ya 100% kila mwaka wa fedha?

Ujenzi na ukarabati wa barabara unasuasua, Mtandao wa Barabara za Lami na changarawe tulionao kwa sehemu kubwa umechakaa na barabara maeneo mbalimbali nchini zimejaa mashimo matupu na kusababisha ajali na usumbufu mkubwa kwa mabasi ya abiria, magari ya mizigo na magari madogo (Fully-Fledged Crisis).

6. JUMUIYA ZA KIMATAIFA

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Shirley Ayokor Botchwey alituma ujumbe maalum mwezi Aprili mwaka 2026 ukiongozwa na Rais Mstaafu wa Malawi, **Dkt. Lazarus Chakwera**, kufanya uchunguzi wa awali. Asante sana Dkt. Chakwera na ujumbe wako kwa kukutana na kufanya mahojiano na wadau wengi muhimu. Mimi binafsi nashukuru kwa kunipatia nafasi ya zaidi ya saa 3 na kuwasilisha maoni na mapendekezo yangu yenye **Kurasa 70**.

Pia itakumbukwa kuwa Bunge la Ulaya mnamo Novemba 27, 2025 na EU na Balozi za Nchi 16 mnamo Disemba 5, 2025 walitoa tamko la kutaka Serikali ikabidhi miili ya marehemu kwa Ndugu ili wakazikwe kwa heshma na kutaka wafungwa wa kisiasa waachiliwe mara moja bila masharti. Leo ni zaidi ya miezi 6 imepita hakuna utekelezaji wowote uliofanywa na Serikali na kwa mantiki hiyo maagizo hayo yamepuuzwa.

Sambamba na hilo Bunge la Ulaya Novemba 2025 lilipitisha maazimio kuitaka Kamisheni ya EU kusitisha mpango wa ufadhili kwa Tanzania wa Euro Milioni 156 (takribani Tsh. Bilioni 438) kutokana na ghasia za uchaguzi na ukandamizaji wa kisiasa na uonevu kwa viongozi wa upinzani.

Licha ya jumuiya za kimataifa kuchukua hatua mbalimbali kutokana na machafuko yaliyotokea Tanzania lakini Jumuiya za Afrika AU, SADC na EAC ziko kimya kana kwamba hakuna kilichotokea. Hadi sasa hakuna kikao chochote kilichoitishwa kwa ajili ya kujadili hali ya kisiasa nchini Tanzania.

Baadhi ya Jumuiya za Kimataifa kama Wabunge wa Kamati Ndogo ya Haki za Binadamu ya Bunge la Ulaya walizuiliwa kuja nchini

kufuatilia machafuko ya Oktoba 2025 jambo ambalo linazidi kuiweka mahala pabaya nchi yetu kidiplomasia.

Muswada wa Sheria umewasilishwa katika Bunge la Seneti la Marekani na Maseneta wawili **Bi**. **Jeanne Shaheen (Democratic Party) na Bw. Ted Cruz (Republican Party)** kuhusu ukandamizaji wa demokrasia na mauaji ya Oktoba 2025 nchini Tanzania ambapo Bunge hilo limeombwa kutoa uamuzi kuiwekea vikwazo nchini yetu katika nyanja mbalimbali jambo ambalo nchi yetu haijawahi kufikia mahusiano mabaya kiasi hicho tangu Uhuru kwani na imekuwa ikitambulika kama kisiwa cha amani.

Maelezo ya Waziri wa Mambo Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, **Balozi Mahmoud Thabit Kombo** kuwa alipeleka barua 25 za Mheshimiwa Rais kwa mataifa mbalimbali duniani za maelezo kuhusu machafuko na mauaji ya Oktoba 2025 ambapo naamini kuwa utetezi huo hauwezi kukubalika mahala popote duniani.

Rais na Serikali yake alishindwa kutoa taarifa rasmi ndani ya nchi ya kilichotokea Oktoba 2025 akidai mpaka iundwe Tume ya Uchunguzi ndiyo ije na majibu lakini pia alitoa msimamo na kauli zinazokinzana na Katiba na Sheria za nchi.

7. UWAZI NA UWAJIBIKAJI KUHUSIANA NA MAUAJI YA OKTOBA 2025

Kutokana na kudhibitiwa kwa vyombo vya habari vya ndani na kuwepo kwa makatazo ya wananchi kutokutoka nje pamoja na kuzimwa mawasiliano ya Intaneti, taarifa za mauaji ziliibuliwa na vyombo vya Kimataifa ikiwemo CNN, DW, BBC, AL JAZEERA, VOA na vyombo vya habari vya nchi jirani hususan nchi ya Kenya.

Kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, suala la usalama na ulinzi wa Raia na mali zao ni jukumu kuu la msingi la Serikali hivyo mauaji ya watu zaidi ya 518 na majeruhi zaidi ya 2,390 kipindi cha uchaguzi wa Oktoba 2025, Serikali haiwezi kukwepa lawama na kuwajibika, ilipaswa Rais na watu wengine wanaohusika wawe wameshawajibika kwa kashfa nzito ya kukatisha maisha ya watu wasio na hatia wakiwemo walemavu, ombaomba, waandishi wa habari, Viongozi wa Dini, wagonjwa, watoto, wajawazito, watu wazima na wazee.

Ni Tanzania pekee katika dunia ya leo ambapo kiongozi mwenye kashfa nzito kiasi hicho anaweza kuendelea kubaki madarakani na kuona ni kawaida tu. Kwa mfano, huko nchini Nepal Kiongozi wa nchi hiyo, KP Sharma Oli amejiuzulu kutokana na kashfa ya vifo vya watu 22 waliouawa katika maandamano ya kupinga ufisadi nchini humo.

Taasisi nyingine ambazo haziwezi kukwepa lawama ya kusababisha machafuko hayo ni pamoja na Msajili wa Vyama vya Siasa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Mahakama ambazo kwa namna moja au nyingine zilishirikiana kwa pamoja kufanya upendeleo na kuharibu uchaguzi kwa kuzuia Vyama na wagombea wa Vyama vya upinzani (ACT WAZALENDO na CHADEMA) kushiriki uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 hususan katika nafasi ya Rais na hivyo kuwanyima wananchi nafasi ya machaguo na hivyo kuamua kuandamana.

Pia Tume ya Uchunguzi ya Jaji Chande haiwezi kukwepa lawama kwa kuliingiza taifa kwenye mzozo mkubwa zaidi kwa kutoa

taarifa kinzani na kuuficha ukweli iliyoufahamu kutokana na ushahidi na vielelezo ilivyopokea kutoka kwa wananchi na Serikali.

Rais na Waziri Mkuu kwa kutoa taarifa zisizoweza kuthibitika na kusababisha hofu, na mkanganyiko mkubwa kwenye jamii. Dhana ya uwajibikaji sio mpya nchini kwetu Viongozi mbalimbali wamewahi kujiuzulu mfano Mzee Ali Hassan Mwinyi na Dkt. Emmanuel Nchimbi (wakiwa Mawaziri wa Mambo ya Ndani), Pia Mheshimiwa Hayati Edward Ngoyai Lowassa (Waziri Mkuu).

Tulimsikia Mtawala anajutia na kusema kungekuwa na uwezekano angetamani siku zirudi nyuma ili yaliyotokea Oktoba 2025 yawe hayakutokea na historia ijiandike upya ili kufuta doa aliloingia, hakika majuto ni mjukuu.

Hakuna uwezekano wa siku kurudi nyuma, wala kurejesha uhai wa watu na viungo vya miili ya binadamu vilivyopotea. Mioyo ya watanzania na familia za wafiwa zinazovuja damu haziwezi kupata faraja kwa maneno ya aina yoyote ya kuomba msamaha isipokuwa Rais mwenyewe kuwajibika.

Rais alikataa ushauri wote uliotolewa na wawakilishi wa wananchi hadi wengine akawafukuza bungeni, Wazee, Viongozi wa Dini, Asasi za Kiraia na Serikali yake ikashindwa kuheshimu hata Mahakama akiamini anaweza kila kitu matokeo yake ndiyo haya wahenga walisema *Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu*.

Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT Wazalendo, **Ndg. Masoud Othman Masoud** ambaye pia alikuwa mgombea wa urais Zanzibar mwaka 2025 alichukua uongozi na kumfuata **Rais Samia Suluhu Hassan** pamoja na Viongozi kadhaa kuwaeleza

juu ya viashiria vya kutokea kwa maafa makubwa nchini lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa hadi kutokea mauaji makubwa ya Oktoba 2025.

Mzee Jaji Joseph Sinde Warioba ambaye alihangaika kumtafuta Rais na Tume Huru ya Taifa Uchaguzi ili kurekebisha kasoro za mifumo ya uchaguzi nchini na kanuni za maadili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ambazo zilikuwa zinakinzana na Sheria na Kanuni za uchaguzi na kwa kufanya hivyo kungeleta maelewano ya pamoja kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 lakini kwa bahati mbaya sana Mzee huyu hakupewa nafasi ya kikao na ushauri wake ulipuuzwa.

Ushauri mwingine uliotolewa na Wazee mashuhuri kama Mzee Samweli H. Kassori, Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Mzee Freeman Aikaeli Mbowe, **Marehemu Suleiman Said Bungara Maarufu Bwege,** Mungu amlaze mahala pema peponi, Mungu ampe kauli thabiti Mzee wetu Ameen. kwa nyakati tofauti tofauti, walishauri namna bora ya kuendesha uchaguzi huru na wa amani ambao nao pia waliishia kudharauliwa.

Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema nanukuu **"Chama kitakachopuuza maoni ya wananchi, kinaweza kikalia kilio asipatikane mtu wa kukisaidia kupangusa machozi, ninachowaambia CCM na waambia Vilevile Vyama vingine, lazima msikilize wananchi wanasema nini**" mwisho wa kunukuu.

CCM inawajibika kwa kuondolewa madarakani kwani hakuna uwezekano tena wa kuendelea kuwa Chama tawala kwa kuwa

Serikali ya awamu ya 6 imekifikisha tamati chama hicho kufuatia machafuko na mauaji ya Oktoba 2025.

8. HITIMISHO

Pamoja na Tume ya Jaji Chande kupata kigugumizi na kushindwa kusema ukweli kuwa Rais akiwa Amiri Jeshi Mkuu na kwa kauli zake zimeacha maswali mengi kuwa huenda yeye ndiye aliyetoa amri ya kuua waandamanaji na raia wengine ambapo ni matumizi mabaya ya mamlaka aliyopewa na Ibara ya 148 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

mfano alikiri hadharani kuwa:-

(i) Mtawala alitamka hadharani kuwa nguvu kubwa iliyotumika ndiyo nguvu iliyotakiwa kuwadhibiti waandamanaji kwani walilenga kupindua Serikali yake na wale wanaolia watoto wao kufa walitakiwa kuwazuia kuandamana.

(ii) Mtawala alisema hadharani kuwa kama isingetumika nguvu kubwa kuwadhibiti waandamanaji hao hali ingekuwa mbaya zaidi ya tuliyoyaona na usalama wa nchi ungekuwa hatarini.

(iii) Serikali ilikataa kutenga muda wa kushiriki mazishi, kuhani misiba, kushiriki Misa za kuwaombea marehemu na majeruhi wala kupeperusha bendera nusu mlingoti kama sehemu ya kuwakumbuka na kuwaenzi mashujaa hao kama ilivyo mila na desturi ya nchi yetu, mfano Rais wa awamu ya 3, **Hayati Benjamin William Mkapa** alitangaza siku 3 za maombolezo na bendera

ya taifa kupepea nusu mlingoti kutokana na ajali ya kuzama kwa Meli ya Mv Bukoba mwaka 1997.

(iv) Wananchi kuzuiwa kutoka nje na kuzima kwa mtandao wa Intaneti kwa siku 6 mfululizo na baadaye kufunguliwa bila kuelezwa sababu za kufungwa.

Matukio hayo ya uvunjifu wa Sheria na Katiba ya nchi huendana na kunyamazishwa kwa vyombo vya habari kwa kufungiwa mfano Jambo Tv, Jamii Forums, Mitandao ya Tiktok, X (Twitter) nk vingine kupigwa faini na waandishi wa habari kupewa misukosuko huku nguvu kubwa zikifanyika kuhamisha wananchi kwenye kujadili ajenda muhimu za kitaifa ili kufunika maovu ya Serikali yasijadiliwe wala kujulikana kwa umma huku kampeni za machawa ndani na nje ya nchi zikishika kasi (Sportswashing)

Serikali haijali ukuu wa Katiba wala Sheria za nchi na inafika mahala hadi Rais kudiriki kusema kuwa ***'Katiba ya nchi ni Kijitabu Tu'*** (Crisis of Consitutional Order and Lawlessness) kinyume na ibara ya 26 (1) na (2) ya Katiba ya nchi mifano michache inayothibisha kwamba Serikali imekuwa ikivunja Sheria na Katiba ya nchi kwa kiwango kikubwa kama ifuatavyo:-

(i) Serikali kuingia mikataba ya siri ya raslimali kinyume cha kifungu cha 12 cha Sheria ya kulinda raslimali na Ibara ya 9 (c), (d), (j), Ibara ya 27 (1), (2) na Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(ii) Kuchukua mikopo nje ya Bajeti na fedha kutokupitia mfuko mkuu wa Serikali na badala yake kuingia kwenye

mifuko ya watu binafsi kinyume na kifungu cha 12 cha Sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348 na marekebisho yake ya mwaka 2020 na Ibara ya 9 (d), (i), (j) na Ibara ya 135 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(iii) Kutapanya fedha za umma na kuruhusu ziliwe kwa urefu wa kamba, Ripoti za CAG kutofanyiwa kazi kikamilifu kinyume na Kifungu cha 38 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura ya 418 na Ibara ya 9 (c), (d) (i), (j) na Ibara ya 27 (1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(iv) Kuvuruga uchaguzi kwa kuruhusu kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi batili na kuminya demokrasia kwa Vyama vya upinzani kinyume na Ibara ya 3, 5 (1), 8 (1) (a), 13 (1), 15 (1) (2) na Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(v) Kushindwa kulinda raia na mali zao na kunyimwa haki za kuabudu kinyume na Ibara ya 9 na 19 (1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vyombo vya uwakilishi wa wananchi kama Bunge na Mabaraza ya Madiwani kudhibitiwa na hata wachache wanaojitokeza kuhoji mambo ya msingi hudhibitiwa kupitia vikao vya Caucus, kupewa taarifa nyingi zisizo na kichwa wala miguu wakati wa uchangiaji ili kupotezewa muda, kunyimwa kuchangia na kusimamishwa vikao na baadaye kufukuzwa rasmi kwenye vyombo hivyo vya uwakilishi wa wananchi. Bunge limekuwa sehemu ya kubariki dhuluma na ufisadi badala ya kuwa chombo cha kulinda maslahi ya umma.

Upande wa Mahakama kuingiliwa na kufanya maamuzi kwa maelekezo ya Serikali na hili Jaji Mkuu amekuwa akilithibitisha mara kwa mara huku mamlaka ya uteuzi wa majaji ikitumika vibaya kufanya upendeleo ili kulinda maslahi binafsi kupitia mhimili huo.

Msajili wa Vyama vya Siasa hajaishia kuingilia utendaji wa Vyama vya upinzani bali pia amekuwa akikataa kusajili Vyama vipya vya Siasa bila sababu za msingi. Mfano **Chama cha Independent People's Party (IPP)** ambapo waanzilishi wa chama hicho wameamua kufungua shauri Mahakamani dhidi ya Msajili wa Vyama vya Siasa baada ya kupigwa danadana kwa miaka 4 wakimlalamikia kunyimwa usajili wa chama hicho licha ya kukamilisha taratibu zote za msingi na hata kulipia ada ya usajili wa muda ya Tsh. Milioni 1.

Pendekezo la kuundwa tume nyingine halikubaliki na hatuwezi kuwa na Tume juu ya Tume tena zinazoundwa na mamlaka ile ile leo Rais ameteua tena tume ya mrengo mmoja anayooita ***'Tume ya Uchunguzi wa Kijinai wa Matukio ya Ghasia ya wakati na baada ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025'.***

Tume ya uchunguzi wa kijinai imechelewa na haiwezi kupewa nafasi tena. Mwanadiplomasia mashuhuri nchini **Profesa Anna Tibaijuka** alishauri mapema kupitia andiko lake tarehe 15 Novemba 2025 katika mtandao wa X akisisitiza kuundwa kwa Tume ya Kijaji 'Judicial Enquiry' lakini ushauri wake ulipuuzwa. Leo Serikali inarejea mawazo yake kwa kuchelewa, haitasaidia. Watanzania na jumuiya za kimataifa haziwezi kusubiri tena.

Katika kipindi cha hivi karibuni Serikali imekuwa na mahusiano mabaya na viongozi wengi wa kisiasa, Viongozi wa Dini, wazee, wanaharakati, Wanahabari hasa wakosoaji ambao wamekuwa wakitungiwa kesi za kubambikwa mara kwa mara ikiwemo Ugaidi na Uhaini na wengine kuzuiwa kugombea kwa nguvu. Hatujasahau kesi za Tundu Lisu, Dkt. Malisa, Heche, Mbowe, Mpina na migogoro kwenye makanisa.

Kama nilivyosema awali Serikali ilishauriwa kikamilifu kabla ya uchaguzi ili isije kusababisha vurugu lakini mfumo mzima wa Serikali ulikaidi na kuendelea na zoezi hilo.

Rais Mstaafu wa awamu ya 4, **Mzee Jakaya Mrisho Kikwete** kwa kipindi chote cha matatizo yaliyolikumba taifa letu amechagua kukaa kimya licha ya Viongozi wa nchi na jumuiya mbalimbali za kimataifa kuja nchini kufuatilia mauaji ya kikatili yaliyofanyika Oktoba 2025. Ukimya wa Mheshimiwa Rais Mstaafu Kikwete umeleta sintofahamu kubwa kwenye jamii na watu kujiuliza kulikoni? huku akionekana mataifa mbalimbali duniani akitafuta suluhu ya migogoro ya kisiasa.

Baada ya kufanya uchambuzi wa muhtsari wa Ripoti ya Tume ya Uchunguzi ya Jaji Chande nimebaini kuwa:-

(i) Muhtasari wa Ripoti ya Tume ya Jaji Chande uliowasilishwa kwa umma ulihaririwa (edited) hadi ukawa skrepa kwa madhumuni ya kuuficha ukweli na kukwepa uwajibikaji, badala yake Tume ikakimbilia kutangaza tuhuma bandia kwa marehemu na watu wengine wasiohusika.

(ii) Waandamanaji waliuawa kwa chuki ya Serikali ya awamu ya 6 kwani walikuwa wanazo haki na kinga kikatiba na kisheria kitaifa na Kimataifa na siyo kweli kwamba walitishia usalama wa nchi na vyombo vya dola kulazimika kutumia nguvu kubwa kama ilivyoelezwa na Tume ya Jaji Chande.

(iii) Serikali ina mgongano mkubwa wa maslahi katika machafuko ya Oktoba 2025 na hivyo ni lazima kitafutwe chombo huru cha nje ya nchi kitakacho tafuta ukweli, kushinikiza uwajibikaji na kusimamia mazungumzo ya amani ili kufikia muafaka wa kitaifa.

(iv) Idadi ya watu waliouawa ni kubwa zaidi ya 518 na watu waliojeruhiwa ni zaidi ya 2,390 tofauti na ilivyoelezwa na Tume ya Jaji Chande kwani Tume hiyo imetoa takwimu zinazokinzana na kuegemea maeneo ya huduma za afya pekee na pia imeacha maeneo mengine muhimu kama Katoro, Geita, Kahama, Tunduma, Bunda, Tarime na Iringa ambayo yaliripotiwa kutokea vifo vingi pia Tume haikuchukua takwimu katika maeneo ya mitaa, vitongoji na vijiji.

(v) Pamoja na Tume ya Jaji Chande kupata kigugumizi kumtaja aliyetoa amri ninaamini mtawala akiwa Amiri Jeshi Mkuu ndiye aliyetoa amri ya kuua na yeye mwenyewe amethibitisha hilo mara kadhaa *(The White Elephant in the room is the head of state).*

(vi) Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ulisimamiwa na Tume batili na isiyo halali kwani haikuwa inatambulika kisheria baada ya kutungwa kwa Sheria mpya ya Tume

Huru ya Uchaguzi ya mwaka 2024. Hivyo iliyojiita Tume Huru ya Uchaguzi ilikuwa ni genge la watu binafsi lililojitwika majukumu ya umma na kusababisha machafuko na mauaji makubwa nchini.

Matokeo hayo ya uchaguzi yalikuwa batili kwani kwa sehemu kubwa kura zilipigwa na maafisa wa Tume Huru ya Uchaguzi badala ya wananchi, kutokana na udanganyifu huo, Tume imeshindwa ku Gazzette matokeo kwenye gazeti la Serikali na hata kwenye tovuti rasmi ya INEC.

(vii) Mahakama ilichangia kwa kiwango kikubwa machafuko ya Oktoba 2025 kwa kuruhusu kufungiwa chama cha Siasa cha CHADEMA kufanya shughuli zake mwaka wa uchaguzi na kuruhusu uchaguzi kuendelea wakati mimi mgombea wa Urais wa ACT Wazalendo nikiwa nimeweka zuio mahakamani la kuzuia uchaguzi kufanyika hadi kesi ya msingi ya kupinga kuenguliwa kwangu itakaposikiliwa na kuamuliwa.

(viii) Waandamanaji walikuwa na sababu za msingi 5 zenye vipengele 20 kama zilivyoanishwa na Tume ya Jaji Chande na sio kweli kwamba walifuata mkumbo kama inavyoelezwa na watawala.

(ix) Bila kudhibiti na kutokomeza kabisa mtandao wa utakatishaji wa fedha haramu, wizi, rushwa, ufisadi, ubadhirifu wa fedha na raslimali za umma, amani na utulivu haiwezi kurejea nchini mwetu.

(x) Uhimilivu wa Deni la Serikali uko kwenye hatari kubwa kwa kuwa deni limeongezeka kwa kasi kubwa na vigezo vilivyowekwa na IMF kwa sehemu kubwa vinakaribia kufikia ukomo na taifa kutokopesheka tena kinyume na taarifa ya Tume ya Jaji Chande inayotuaminisha kuwa taifa liko kwenye kiwango cha kuaminika katika ukopaji kutokana na tathmini ya Moody's.

(xi) Mfumko wa bei za bidhaa na huduma, ugumu wa maisha pamoja na changamoto nyingine zilizopo ni za kutengeneza kwa maslahi ya mafisadi wachache zitakomeshwa muda mfupi baada ya kupata Viongozi bora katika taifa.

(xii) Madai ya Tume ya Jaji Chande kuwa mali zilizoharibiwa na kufikia hasara ya Tsh Bilioni 125 hayana uhalali kwani hakuna uthibitisho wa kuhakikiwa na chombo chochote chenye mamlaka kisheria kama RITA na Mthamini Mkuu wa Serikali

(xiii) Tume ya Jaji Chande kwa siku 153 imeshindwa kukokotoa na kubainisha fidia kwa marehemu na watu waliojeruhiwa, hasara waliyopata wananchi kutokana na kuzuiwa kutoka nje na kuzimwa kwa mtandao wa intaneti kwa siku 6 mfululizo.

(xiv) Maelezo ya Tume ya Jaji Chande yamekinzana na Kauli nyingi za Rais na Waziri Mkuu lakini pia kauli zingine zimeshindwa kuthibitika kama ambavyo viongozi hao waliibua tuhuma mbalimbali dhidi ya waandamanaji.

(xv) Ninaungana na pendekezo la Tume kuwa ni lazima kuwepo Baraza la wazee (Fuddy-duddy depository) katika uendeshaji wa nchi ingawa hata wazee wachache wanaojitokeza hadharani kutoa maoni yao wanapuuzwa na Serikali ya awamu ya 6.

(xvi) Tume imeukingia kifua mtandao wa utekaji, upotezaji na mauaji ya wananchi wasio na hatia kwa kushindwa kusema ukweli sababu za kutekwa na kuuawa na hatua zinazochukuliwa licha ya kuripoti idadi kubwa ya watu 758 waliotekwa na kupotea katika kipindi cha miaka 3 kuelekea uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 na kati ya hao watu 245 hawajulikani walipo hadi sasa.

(xvii) Ongezeko la muda wa siku 63 ya Tume ya Jaji Chande kufanya kazi halikuwa na uhalali kisheria na pengine lililenga kupoteza muda, kuchakachua ripoti na kufuja fedha za umma.

(xviii) Nilienguliwa kugombea nafasi ya Rais katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa mabavu na kinyume cha sheria na Msajili wa Vyama vya Siasa, INEC na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kumfanya mgombea wa CCM Samia kukosa ushindani.

(xix) Tundu Antipas Lissu, Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA kufunguliwa kesi ya mchongo ya uhaini na Chama chake kufungiwa kufanya shughuli za kisiasa ililenga kumdhibiti yeye na Chama chake asishiriki uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ili kuipa ahueni CCM.

(xx) Ninapinga kuanzishwa kwa Tume nyingine chini ya mamlaka hiyo hiyo ya Rais kwani haitokei kuunda tume mbili kwa madhila yanayotokana na tukio moja, hii ni kuwapotezea muda wananchi, kufuja fedha za umma na ni ujanja wa kukwepa mchakato wa Mahakama ya Uhalifu (ICC) na mamlaka zingine za kimataifa.

Rais amekimbia na Ripoti ya awali na Tume imeshindwa kuweka wazi gharama ilizotumia kufanya kazi zake lakini bila aibu imependekeza kuundwa tena kwa Tume nyingine.

(xxi) Mtawala hataki Viongozi na watumishi wanaotekeleza vyema majukumu yao kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi na ndio maana amekuwa na utamaduni wa kubadilisha watendaji na viongozi waandamizi serikalini kama nguo, lakini pia wazembe na mafisadi wanazawadiwa vyeo kila uchao. Hii inaleta hisia kuwa mtawala huyu huenda halitakii mema taifa letu la Tanzania.

(xxii) Licha ya wezi wa fedha za umma kufahamika kwa majina na vyeo vyao ndani ya Serikali, mamlaka za mashtaka,upelelezi na uchunguzi za DPP, DCI na TAKUKURU zimeshindwa kuwakamata na kuwafungulia mashtaka na inapobidi kutaifisha mali zao.

(xxiii) Taifa limepata anguko kubwa kutokana na Taasisi nyingi za umma na Kijamii kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa uhuru kutokana na taasisi hizo kujaa machawa na makachero mfano

Bunge, Mahakama, INEC, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Vyama vya Siasa, Vyama vya Wafanyakazi, Serikali za Wanafunzi wa Vyuo vikuu, Jumuiya za Wafanyabishara, Vyama vya Wakulima na Wafugaji nk.

(xxiv) Rais hana mamlaka kikatiba na kisheria kuzuia ripoti ya umma na hivyo kitendo cha Rais kudai ripoti ya Tume ni mali yake na isidaiwe na mtu yoyote ni uvunjaji mkubwa wa Sheria na Katiba ya nchi na kukwepa uwazi na uwajibikaji.

(xxv) Haitawezekana kuwepo kwa maridhiano bila ya ukweli kuwekwa wazi (Fact Findings) na Uwajibikaji kwa yaliyotokea Oktoba 2025 tofauti na mapendekezo yanayotolewa na Tume ya Jaji Chande ya kuundwa Tume ya Maridhiano.

(xxvi) Hadi sasa zaidi ya miezi 7 imepita hakuna aliyewajibika ni danadana tu na kuundiwa tume juu ya tume. Imekuwa ni jambo rahisi zaidi kwa nchi yetu kushtakiwa katika Mahakama za Kimataifa ICSID ili kuhalalisha uuzaji wa raslimali za nchi lakini imekuwa vigumu Viongozi kuwajibika ICC.

(xxvii) Tume za Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola iliyoongozwa na Dkt. Lazarus Chakwera, Rais Mstaafu wa Malawi, ripoti yake inasubiriwa kwa hamu kubwa na watanzania na tunaamini kuwa itakuwa rejea muhimu kwa hatua za uwazi na Uwajibikaji.

(xxviii) Jumuiya za Afrika AU, SADC na EAC kushindwa kushughulikia migogoro na machafuko kiasi kwamba

matatizo ya Afrika yanashughulikiwa zaidi na Jumuiya za Kimataifa badala ya Afrika yenyewe. Kutoa adhabu ya kuondolewa kwenye jumuiya nchi ambazo zimepinduliwa kijeshi (Military Coup), lakini kwa viongozi walioingia madarakani kwa kumwaga damu za watu, wizi wa kura na ukandamizaji mkubwa wa demokrasia jumuiya hizo hazijishughulishi kabisa na matatizo hayo.

Sababu kuu 5 zenye vipengele 20 zilizoanishwa na Tume ya Jaji Chande kuwa chanzo cha maandamano zinauzito mkubwa na ni dhahiri kuwa waandamanaji walikuwa na sababu za msingi za kuandamana na hawakufuata mkumbo kama ambavyo Tume inajaribu kutoposha, hongera sana Gen-Z, hongera sana waandamanaji wote mmejitoa bila kujibakiza kwa taifa lenu, wengine mmepoteza maisha, wengine mmepoteza viungo vya mwili na kuwa na ulemavu wa kudumu, historia ya nchi yetu haitawasahau orodha yenu ipatikane na iunganishwe na mashujaa wengine waliolipigania taifa letu.

Watanzania wanahitaji Viongozi wenye weledi na uwezo wa ziada (Will-power) kuwapeleka kwenye mafanikio ya kweli, Maandamano ya Oktoba 2025 ni ishara ya watanzania kuchoshwa na Serikali hii iliyoshindwa kuwajibika kikamilifu na ndio maana walisikika wakiimba na kusema ***hatumtaki mama Samia***, **hatuitaki CCM na tumechoshwa na ufisadi nchini**, **tunataka nchi yetu,** wengine walisikika wakisema, **Ndugu zetu wametekwa sana, wameuawa sana na wengi hawana familia, tukaona watanzania kwa pamoja tuungane, tushirikiane hatumtaki Rais Samia, tunataka nchi yetu**

Watanzania wamechoka kudhulumiwa, kuibiwa fedha na raslimali za umma, maisha magumu, kutekwa, kupotezwa na kuuawa, ndiyo maana walisimama kulipigania taifa lao na ili kurejesha hesma palipojaa dharau. Mungu azilale roho za mashujaa hawa na uwakumbuke siku ya mwisho angalia link **https://youtu.be./buc2bdkBtmg?si=x-bNMqV-Rfl2Mu na https://youtu.be/m4hWpd-kFM?si=JYbbA0CLDl43c7MM**

Raha ya Milele, Uwape eeh Bwana na Mwanga wa Milele uwaangazie, Wapumzike kwa amani. Amina,

Ina Lillahi wa inna Ilayhi Raji'un.

9. MAONI NA MAPENDEKEZO

Baada ya kufanya uchambuzi hapo juu ninatoa Maoni na mapendekezo kama ifuatavyo:-

(i) Kuundwa Tume Huru chini ya Umoja wa Mataifa (UN), Jumuiya ya Madola (Commonwealth) na Umoja wa Ulaya (EU) itakayohusisha makundi yote muhimu ya ndani na ya nje ya nchi kufanya uchunguzi kwa uwazi na bila upendeleo wa upande wowote.

(ii) Kulipa kifuta machozi kwa familia zote za marehemu na fidia na vifaa saidizi kwa watu wote waliopoteza viungo vya mwili. Pia kuwarejesha watu 245 ambao hawajulikani walipo hadi sasa.

(iii) Rais, Msajili wa Vyama vya Siasa, INEC, AG, Mahakama na wengine waliohusika wawajibike kwa kashfa ya kusababisha vifo vya watu zaidi ya 518 na majeruhi zaidi ya 2,390 wasio na hatia ili kuliponya taifa na

kudumisha Uwajibikaji (*naungana na Maoni ya Tume kuwa asiwepo mtu wa kutolewa kafara-Sacrificial Lamb*)

(iv) Vyombo vya Dola vikiongozwa na **Afande CDF** vimtake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na aliyekuwa Waziri wa Fedha (Waziri Mkuu wa sasa) waeleze yalipo matrilioni ya fedha za umma yaliyoibwa na kufujwa, pia vyombo hivyo viwatake Viongozi hao kuweka wazi jedwali la mikopo na mikataba yote ya raslimali iliyoingiwa kwa siri katika kipindi cha uongozi wao wa miaka 5 iliyopita.

Aidha na ifahamike kuwa jukumu la kwanza la msingi la Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ni kulinda Katiba na Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(v) Tume huru ya kimataifa itakayoundwa pamoja na mambo mengine ichunguze ukwasi wa baadhi ya Viongozi wanaotuhumiwa kuiba na kuficha fedha za umma nje ya nchi na kusaidia kutaifisha mali na fedha hizo na kuzirejesha nchini na hii ifanyike kwa kuhusisha Taasisi zinazoaminika kimataifa za uchunguzi wa fedha (Accredited Financial Investigators-AFI).

(vi) Watanzania wote wazalendo na wenye mapenzi mema na nchi yetu walioko ndani na nje ya nchi wanaombwa kufichua mitandao ya wizi na kuweka wazi nyaraka zinazohusu ufisadi ili umma uweze kuchukua hatua stahiki za uwajibikaji.

(vii) Uchaguzi wa tarehe 29 Oktoba 2025 ufutwe na kutangazwa uchaguzi mpya ili kuwapa nafasi wananchi kuchagua Viongozi wanaowataka katika ngazi ya Rais, Wabunge na Madiwani ili kurejesha umoja, mshkamano, amani na utulivu nchini.

(viii) Kesi ya kupinga kuenguliwa kugombea Urais iliyopo Mahakama ya Rufaa kati yangu mimi Luhaga Joelson Mpina na ACT Wazalendo dhidi ya INEC na AG. Pia kesi kati yangu mimi Luhaga Joelson Mpina na ACT Wazalendo dhidi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (RPP) na AG.

Aidha kesi nyingine ni kati ya ACT Wazalendo dhidi ya INEC na AG kuhusu uteuzi wa wabunge wa Viti Maalum zisikilizwe na kuamuliwa haraka ili kutenda haki na kuwa rejea muhimu katika safari ya ujenzi wa demokrasia nchini.

(ix) Wakati shauri likiwa Mahakama ya Rufaa kusubiri kusikilizwa na kuamuliwa Chief Justice, Mheshimiwa Masaju ajitokeze hadharani kuueleza umma wa watanzania na dunia kwa ujumla status yangu ni ipi kwa sasa kwani nimekaa kwenye ugombea wa Urais wa kudumu na endelevu muda mrefu, kwa kuwa yeye ndiye aliye na kesi yangu na yeye ndiye aliyeshuhudia kiapo cha Mtawala katika Kambi ya Kijeshi badala ya Uwanja wa Jamhuri Dodoma kama ilivyozoeleka miaka yote.

(x) Mahakama iache kutumika kisiasa na kuwa sehemu ya kutakatisha uhalifu na kuwanyima haki wenye haki na badala yake ijijenge upya kama ilivyokuwa enzi za Jaji Mkuu, Hayati Fransis Lucas Nyalali.

(xi) Liundwe Baraza la Taifa la Katiba ambalo litateuliwa na wananchi wenyewe badala ya Bunge la Katiba linaloteuliwa na Rais, Katiba ya Wananchi haiwezi kuandikwa na wateule wa Rais na Viongozi wa Chama cha Mapinduzi. Ripoti ya Tume ya Jaji Warioba itumike kama rejea na funzo kubwa. Katiba mpya ipatikane mapema mwaka 2027 badala ya mwaka 2028 ilivyopendekezwa na Tume ya Jaji Chande.

(xii) Vyuo vikuu vya nchi yetu viruhusu midahalo ya Wasomi ambayo italiokoa taifa kama tulivyoshuhudia hivi karibuni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete akiwa Chuo Kikuu cha Havard Marekani anatoa mhadhara kwenye mdahalo lakini chuo chake midahalo haifanyiki kama ilivyozoeleka miaka ya nyuma katika ukumbi wa Nkrumah (Nkrumah Hall) ambao ndio uliokuwa chemchem ya mageuzi ya kifikra nchini.

Mwisho nimalizie kwa kutoa masikitiko yangu juu ya Raslimali za taifa letu ambazo tumezilinda kwa machozi, jasho na damu na wivu mkubwa tangu Uhuru mwaka 1961, leo zinauzwa na kumilikiwa na watu binafsi tena kwa siri. Fedha za umma zinatapanywa na kupelekea huduma za Kijamii na Kiuchumi kwa wananchi kudorora. Kwa mwendo huu watoto na wajukuu wetu watakuja kurithi nini?

Kwa nchi yetu ilipofikia kwa sasa lawama hizi tunapaswa tuzibebe watanzania wote kwa kutotimiza Wajibu wetu kikamilifu tuliopewa na Katiba na kuingia kwenye mtego wa ushabiki uliopitiliza wa Vyama vya Siasa na michezo, Vyama vya upinzani kukosa umoja na mshikamano na mambo ya kung'ata na kupuliza hivyo kushindwa kutimiza wajibu wao kikamilifu katika kuisimamia Serikali.

Wazee ni mizizi na shina la ustawi wa taifa letu. Nchi yetu imebaki yatima hasa baada ya Wazee wengi na wenye uzoefu mkubwa waliowahi kushika nyadhifa za juu kwenye Utumishi wa umma kuchagua kunyamaza hata pale mambo yanapoharibika hii ni kutokana na Viongozi hao kukosa uzalendo na kutegemea fadhila ya teuzi za mtawala na kuliacha taifa linaangamia.

Pia nashindwa kujizuia kuwapongeza sana Viongozi wetu wa Dini ya Kiislamu na Kikristo kwa kuwa na msimamo thabiti na kukataa kuyumba wala kuyumbishwa katika kipindi hiki kigumu nchi yetu inapitia. Aidha nawapongeza wazee wetu Jaji Joseph Sinde Warioba, Profesa Anna Tibaijuka, Mzee Samweli Kasori kwa msimamo thabiti. Pamoja na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Aidha pamoja na yote tunayopitia kwa sasa kama taifa niwaombe Ndugu watanzania wenzangu tujipe moyo ushindi unakuja na kwamba **YANA MWISHO HAYA.**

Asanteni kwa kunisikiliza,

Luhaga Joelson Mpina
Aliyekuwa Mgombea Urais kupitia Chama cha ACT
Wazalendo mwaka 2025